# Nipashe

Jumatatu Agosti 1, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581024

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII



The Guardian digital

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US



BREAKING NEWS

SUPA JACKPOT

1,019,301,493/-

KWA 1000/- TU!

SportPesa.CO.TZ PIGA *150*87#




**Kundi** la nyuki lazua taharuki, lavamia shule na kujeruhi walimu...

UKURASA 5



MANE ATAKA MATAJI ZAIDI BAYERN

UKURASA 22




Baadhi ya wakazi wa Mbezi Mwisho Manispaa ya Ubungo jijini Dar es Salaam wakifanya shughuli zao za kuuza mboga za majani chini ya bango la TANROADS linalozuia kufanya biashara kwenye eneo hilo jana. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Rafu CCM zafuta uchaguzi

• **Wajumbe** washtukia wateule kupita bila... *Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 3

**MWAKA MPYA WA KIISLAMU KUTANGAZWA SIKU YA MAPUMZIKO**

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Alhaj Dk. Hussein...

UKURASA WA 4

RIPOTI MAALUM

**MAMBO 12 YA KUZINGATIA KABLA YA KUENDESHA GARI**

MAENEO 12 muhimu yametajwa ambayo dereva anatakiwa kuzingatia...

## Aweso achukizwa, avunja Jumuiya Watumiaji Maji

UKURASA 8



Wananchi wa Mto wa Mbu wilayani Monduli mkoani Arusha wakiwa na ndoo, mabango na matawi ya miti baada ya kuzuia msafara wa Waziri wa Maji, Jumaa Aweso jana, wakilalamikia kero ya maji katika eneo hilo. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

## NEMC yatoa mwezi mitambo ya dhahabu kuondolewa

UKURASA 2


MICHEZO SIMBA HAIZUILIKI, HAISHIKIKI – BARBARA UK.24 MAONI, KATUNI UK.6



Askari akisimamia ubomoaji wa nyumba katika eneo la Kimbesa Mpijimagohe Manispaa ya Ubungo mkoani Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Rafu CCM zafuta uchaguzi

**Na Richard Makore, MWANZA**

SIKU chache baada ya wanachama zaidi ya 400 wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Kata ya Mahina wilayani Nyamagana mkoani Mwanza, kutishia kurudisha kadi za chama hicho kutokana na kasoro mbalimbali za uchaguzi wa mashina 80 na matawi manane katika eneo hilo umefutwa rasmi.

Miongoni mwa kasoro zilizolalamikiwa ni pamoja na ukiukwaji wa kanuni za uchaguzi huo kwa kuteua viongozi badala ya kuwachagua kama kanuni za CCM zinavyoelekeza.

Akizungumza na Nipashe jana Katibu wa CCM Wilaya ya Nyamagana mkoani Mwanza, Geofrey Robert, alisema uchaguzi huo umefutwa baada ya kuwapo malalamiko ya ukiukwaji wa kanuni zinazosimamia uchaguzi.

Alisema licha ya kuwapo malalamiko katika kata zingine wilayani humo, lakini Kata ya Mahina yalikuwa mengi ndiyo maana walichukua hatua haraka na utafanyika baada ya kukamilika taratibu za ndani.

Kutokana na hatua hiyo, Robert alisema uchaguzi ngazi ya kata hiyo hautafanyika kama ilivyopangwa hadi hapo uchaguzi wa mashina na matawi utakapofanyika.

"Kanuni za uchaguzi zilikiukwa kwa kiasi kikubwa katika uchaguzi ule na wanachama wetu walilalamika na kwa kuwa sisi ni chama kikubwa tuliamua kuchukua hatua hii," alisema Robert.

Hali hiyo imejitokeza ikiwa ni miezi minne tangu uongozi wa CCM Taifa kupiga marufuku upangaji wa safu za uongozi ndani ya chama hicho kwa kuangalia uchaguzi mkuu wa 2025.

Aprili 10, mwaka huu, Makamu Mwenyekiti wa CCM Taifa, Abdulrahman Kinana na Katibu Mkuu wake, Daniel Chongolo, waliwataka wanachama wanaopanga safu kuacha mara moja kwa kuwa hawatafanikiwa na hatua zitachukuliwa dhidi yao.

Walisema viongozi wanaopanga safu ya watu wanaowataka hawana nia njema ya kusukuma gurudumu la maendeleo mbele, huku wakisisitiza ni haki ya mwanachama kuchagua na kuchaguliwa.

Licha ya uchaguzi huo kufutwa, baadhi ya wanachama wa eneo hilo walioulalamikia wamedaiwa kuitwa katika kamati za maadili na kutishwa, huku wakidai kupangwa kwa safu za uongozi jambo ambalo ni kinyume na kanuni.

Akizungumzia suala hilo, Robert alisema kila mwanachama ana haki ya kusikilizwa na kwamba haki lazima itendeke kwa kufuata kanuni na taratibu za uchaguzi na siyo kutishwa.

Wiki iliyopita wanachama wa CCM katika kata hiyo akiwamo, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi katika Kata ya Mahina, Patrick Brakari, alisema uchaguzi huo ngazi ya mashina na matawi umeshafanyika katika maeneo mengine, lakini wameshangaa kuona viongozi walipatikana kwa kuteuliwa badala ya kuchaguliwa.

Aidha, alisema haijulikani nani aliteua viongozi hao kwa kuwa kama kiongozi wa kata hajawahi kuona wala kushiriki chaguzi hizo, na hajui walipatikanaje.

Aliongeza kuwa kutokana na sakata hilo, wanachama walikasirika na kutishia kurudisha kadi zao za chama kama haki isingefanyika, ikiwamo kuitishwa uchaguzi kwa kufuata katiba.

Brakari alisema kwenye kata yake ilitolewa fomu moja kwa kila nafasi, hatua inayowanyima wengine nafasi kwa kuonyesha waliojaza wamepita bila kupinga.

Alifafanua kuwa Katiba ya CCM inataka kila mtu apigiwe kura hata kama yupo peke yake, ipigwe kura ya ndiyo ama hapana, lakini kilichotokea wao walipelekewa majina ya wateule ambayo walichagua wenyewe na siyo kuchaguliwa na wanachama.

"Kata ya Mahina kuna rafu za ajabu kabisa, yaani mimi ni kiongozi ngazi ya kata, lakini sijui uchaguzi wa mashina na matawi ulifanyika lini, wapi na ulisimamiwa na nani," alihoji Brakari.

Kutokana na sakata hilo, alisema yeye pamoja na wanachama wenzake waliandika barua wilayani kulalamika kuhusu sakata hilo.

Aliongeza kuwa kuna viongozi wa ngazi mbalimbali wanapanga safu za wanachama watakaowapigia kura na kwamba hiyo ndiyo sababu kwenye kata hiyo viongozi wa mashina na matawi wameteuliwa badala ya kuchaguliwa.

Akizungumza na Nipashe kuhusu sakata hilo, Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya ya Nyamagana, Zebedayo Athuman, alithibitisha kufahamu mgogoro huo ambao alisema ni wa muda mrefu.

Alipoulizwa kuhusu wanachama kutaka kurudisha kadi za chama kutokana na kuteuliwa viongozi wasiowataka, alisema hahusiki na suala hilo.

Alisema wanachama wa mashina, matawi na kata ya Mahina wilayani Nyamagana walifikisha suala hilo ngazi ya wilaya, ingawa hakutaka kusema uamuzi gani ulitolewa kwa wakati huo.

Uchaguzi wa mashina na matawi ndani ya CCM ulianza Aprili 2, mwaka huu, na sasa unahitimishwa kwa wagombea kupigiwa kura na wanachama halali.

# NEMC yatoa siku 30 mitambo uchenjuaji dhahabu iondolewe

**Na Mwandishi Wetu, NZEGA**

BARAZA la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira nchini (NEMC), limetoa siku 30 waliojenga mitambo ya kuchenjulia dhahabu kwenye makazi kuondoa na watakaokahidi watalipa faini ya Sh. milioni 10 hadi Sh. bilioni 30.

Hatua hiyo imekuja baada ya NEMC kushtukia wimbi la ujenzi wa mitambo ya kuchenjulia dhahabu kwenye makazi ya watu hali inayohatarisha afya za wananchi kutokana na sumu iliyomo.

Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, alitoa kauli hiyo jana katika ziara wilayani Nzega mkoani Tabora ya kukagua na kuhakikisha mazingira yanahifadhiwa.

Alibainisha kuwa mitambo hiyo inatoa sumu inayoleta madhara kwa binadamu.

"Kumejitokeza wimbi kubwa sana la mitambo tunaita ya 'elusion' kama mnavyoona hapa inapika au inachemsha dhahabu kwenye maeneo ya makazi, tatizo kubwa mitambo ya aina hii inatakiwa kuwa kwenye maeneo ya migodi kule ambapo dhahabu inachimbwa au eneo ambalo una leseni kabisa ya uchenjuaji madini," alisema.

Dk. Gwamaka alisema maeneo yaliyobainika kuwa na mitambo hiyo kwenye maeneo ya makazi ni Nzega, Geita, Chunya na Tarime.

Alisema katika uchenjuaji kuna kemikali ambazo zinahitaji miundombinu ya kuhifadhi, ili zisiende kwenye mazingira.

"Kwa miaka ya hivi karibuni kumejitokeza wimbi kubwa la mitambo hii kujengwa maeneo ya watu, kuna halmashauri zimefanya vizuri zimetenga maeneo ya viwanda ambayo ndio hiyo mitambo inatakiwa kuwapo," alisema.

"Kimsingi hizi kemikali za sumu mtu anavyovuta zinaathiri mapafu yake na afya kwa ujumla na hata ukifanya kazi kwenye mitambo lazima uvae mavazi ya usalama ili kukinga mwili wako."

Mkurugenzi huyo alisema dhahabu inapopikwa kwenye mtambo huo na moshi unaotoka nje unawakumba watu ikiwamo wapita njia na majirani wa eneo hilo kwa kuwa hawana vitu vya kuzuia hali hiyo.

"Tumetoa mwezi mmoja hadi Septemba mosi, mwaka huu iondolewe kwenye maeneo ya makazi na baada ya hapo tutafanya ukaguzi na tukikuta huo mtambo unafanya kazi adhabu ipo wazi kisheria utajiandaa kulipa kati ya Sh. milioni 10 hadi Sh. bilioni 10, tutaangalia kosa lako lina ukubwa gani," alibainisha.

Alisema NEMC haiwezi kuvumilia wananchi wakiathiriwa afya zao wakati wana haki kikatiba ya kuishi kwenye mazingira bora na salama.

Aidha, Tanzania ni miongoni mwa nchi zilizotia saini Mkataba wa Minamata unaohusu zebaki wa kupunguza matumizi ya kemikali hiyo kwa wachimbaji wadogo, wastani wa asilimia 30, pia kuongeza uelewa wa jamii ifikapo mwaka 2025.

Lengo kuu ni kuokoa afya za wachimbaji wadogo wa dhahabu, pia kulinda mazingira nchini kwa kuwa inayotumiwa na wachimbaji wadogo hupotelea kwenye mazingira kwa asilimia 64 na kwenye hewa wakati wa uchomaji asilimia 36.

Ili kufikia lengo hilo, Wizara ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), iliandaa mpango unaongalia hali ya sekta na wachimbaji wadogo, malengo muhimu, mkakati wa utekelezaji ama kupunguza au kuufuta.

Mpango uliopo kati ya mwaka 2020 na 2025, unaeleza shughuli za wachimbaji wadogo, kuondoa kemikali zilizoko kwa miaka 100 sasa na tathmini inaonyesha takribani tani 13.2 hadi 24.4 za zebaki hutumika kila mwaka katika uchenjuaji wa dhahabu.

Mtaalamu wa Mazingira kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), Kamkuru Maganya, alisema zebaki kwa kiasi kikubwa inaingizwa nchini kwa njia zisisizo rasmi, akitaja mipaka ya Sirari na Namanga, ambako ndiko kwenye upenyo mkubwa.

Ofisa huyo pia anaitaja bandari bubu iliyoko Dar es Salaam, nayo inachangia asilimia 25 na asilimia 20 katika mpaka wa Tunduma, Songwe.

HABARI KITAIFA

# Mwaka mpya wa kiislamu kutangazwa siku ya mapumziko

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Alhaj Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema kuwa serikali itatoa tamko kuifanya siku ya mwaka mpya wa Kiislamu kuwa ya mapumziko. Rais Mwinyi aliyasema hayo jana katika kongamano la maadhimisho ya mwaka mpya wa Kiislamu 1444, lililofanyika msikiti wa Jamiu Zinjibar, Mazizini, Mkoa wa Mjini Magharibi.

Aidha, alisema maadhimisho hayo yatafanyika kwa mzunguko kati ya Unguja na Pemba ili kutoa nafasi kwa Waislamu kushiriki.

Aliipongeza ofisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar kwa kuandaa maadhimisho hayo ambayo ni utaratibu mpya kufanyika visiwani hapo na inatoa fursa kwa waislamu kujua mwaka wao kwa mujibu wa tarehe za dini yao.

"Hakuna asiyeujua mwaka mpya ule wa kawaida na siku ya mwaka mpya ikifika basi kila mtu anajua lakini kwa bahati mbaya sana mwaka mpya wa kiislamu watu wengi hawautambui," alisema. Alisema utaratibu wa kuadhimisha mwaka mpya wa kiislamu utawakumbusha Waislamu kuujua. Aidha, aliwakumbusha wananchi kushiriki zoezi la sensa ya watu na makazi Agosti 23, mwaka huu kutokana na umuhimu wake katika kupanga maendeleo ya nchi.

Naye Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman, alimwomba Dk. Mwinyi kuifanya siku ya mwaka mpya wa kiislamu kuwa ya mapumziko ili waumini wa dini hiyo wapate fursa ya kusherehekea na familia zao kama zilivyo sikukuu nyingine.

Mapema Mratibu Mkuu wa Kongamano hilo, Shekhe Khalid Ali Mfaume, alisema lengo la maadhimisho hayo ni kuwakumbusha waislamu wajibu wao wa kujua tarehe za uislamu.

Alisema Sheria namba nne ya Ofisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar ndiyo iliyowezesha kufanyika kongamano hilo pamoja na shughuli nyingine zilizoandaliwa.

Akitoa mada kuhusu sensa na uislamu, Shekhe Khamis Abdulhamid, alisema sensa imetajwa ndani ya Quran na uislamu haukatazi watu kuhesabiwa kwa kuwa ni muhimu kwa sababu inasaidia kupanga maendeleo ya baadaye.

Alisema, sensa maana yake ni kujua idadi ya watu na makazi yao na namna walivyo katika maendeleo ya kiuchumi.

Kongamano hilo pia lilihudhuriwa na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Massoud Othman, Makamu wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdalla na viongozi wengine wa vyama na serikali.

**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**
**(COMMERCIAL DIVISION)**
**AT DAR ES SALAAM**

**COMMERCIAL CASE NO. 60 OF 2022**

**CRDB BANK PLC....................PLAINTIFF**

**VERSUS**

**GREENS CONSTRUCTION LTD...................1ST DEFENDANT**
**HAMIMU HUSSEIN BAKARI.......................2ND DEPENDANT**
**ERNEST SAMSON LAIZER........................3RD DEPENDANT**
**HAMIS BAKARI LUZIGA.............................4TH DEPENDENT**

**SUBSTITUTED SERVICE BY PUBLICATION**

**TAKE NOTICE** that the plaintiff has instituted a suit against you upon the claim the particulars of which are set in the plaint service of the summons in you has ordered by means of publication. You are directed to collect copies of the application documents from the court's Registry, P.O. Box 12533, Dar es salaam. The 2nd, 3rd and 4th Defendants are required to **file Written Statement of Defence by 30th August, 2022** and you are hereby summoned to appear in this court in person or by an Advocate or an agent duly authorized on **12th September, 2022 at 10:00am before Hon. Z.A. Maruma, Judge for First PTC. TAKE FURTHER NOTICE THAT** should you default to enter appearance as herein provided, the matter will proceed and decision may be given in your absence.

Given under my hand and Seal of the Court this 28th day of July, 2022.

DEPUTY REGISTRAR
COMMERCIAL DIVISION
DAR ES SALAAM

116970802




## TAARIFA KWA UMMA

**HAKI ZA KURUSHA MATANGAZO MBASHARA YA ENGLISH PREMIER LEAGUE, UEFA CHAMPIONS LEAGUE, UEFA EUROPA LEAGUE, UEFA EUROPA CONFERENCE LEAGUE, UEFA SUPER CUP, COMMUNITY SHIELD, SERIE A, LA LIGA, UEFA YOUTH LEAGUE, FA CUP NA FIFA WORLD CUP 2022 MSIMU WA 2022/2023 NDANI YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

SuperSport International (Pty) Limited, ni moja ya kampuni tanzu ndani ya Kundi la Makampuni ya MultiChoice inayowakilishwa hapa nchini na kampuni ya MultiChoice Tanzania Limited, ambayo inasimamia huduma kwa wateja wa MultiChoice katika eneo la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

MultiChoice Tanzania inapenda kutoa TAARIFA kwa wamiliki wa mitandao ya kurusha matangazo kwa njia ya waya (Cable), makampuni ya utangazaji na umma kwa ujumla, kuwa SuperSport International (Pty) Limited, inahodhi haki za kurusha matangazo (exclusive Pay Tv broadcast rights) ya mashindano yafuatayo:

1. ENGLISH PREMIER LEAGUE
2. UEFA CHAMPIONS LEAGUE
3. UEFA EUROPA LEAGUE
4. UEFA EUROPA CONFERENCE LEAGUE
5. UEFA SUPER CUP
6. UEFA YOUTH LEAGUE
7. FA CUP
8. FIFA WORLD CUP 2022
9. COMMUNITY SHIELD
10. SERIE A
11. LA LIGA

Matangazo ya mashindano hayo yanaruhusiwa kurushwa kupitia Chaneli za SuperSport pekee ambazo hupatikana katika kisimbuzi cha DStv kinachoendeshwa na MultiChoice Group (MCG). Haki hizi ni kwa ukanda wote wa Afrika – Kusini mwa Jangwa la Sahara na visiwa jirani (Sub-Saharan Africa and adjacent islands) ikiwemo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kwa minajili hiyo, kurusha, au kusambaza kwa njia yoyote ile matangazo ya mashindano hayo katika eneo tajwa bila idhini ya MultiChoice ni kinyume cha sheria, kanuni na makubaliano ya haki miliki.

Tunaujulisha umma kuwa MultiChoice na washirika wake, hawatasita kuchukua hatua kali za kisheria kwa yeyote atakayerusha matangazo ya mashindano hayo bila idhini.

Imetolewa na:

MultiChoice Tanzania Limited kwa niaba ya MultiChoice Group
Julai 26, 2022

RIPOTI MAALUM

# Mambo 12 ya kuzingatia kabla ya kuendesha gari

**Na Romana Mallya**

MAENEO 12 muhimu yametajwa ambayo dereva anatakiwa kuzingatia kabla ya kuendesha gari ili kuhakikishia usalama wake binafsi na abiria atakaowabeba katika chombo chake.

Kaimu Mkuu wa Idara ya Usalama katika Usafirishaji na Mazingira (TSES) wa Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), Mhandisi Patrick Makule, aliyataja maeneo hayo kuwa ni ukaguzi wa tangi la mafuta, matairi, wiper (kifuta maji), taa, dashi bodi (Dash Body), usukani, breki, kuangalia oil ya injini na gia, milio kwenye gari, viti na mikanda.

Mtaalamu huyo anayakumbusha hayo ikiwa ni siku moja kupita baada ya ajali iliyotokea Mjimwema, Kata ya Magengeni, Mtwara na kuua 13 kati yao wanafunzi wakiwa tisa na kujeruhi 17.

Ajali hiyo ilitokea baada ya basi la shule kutumbukia kwenye korongo, huku chanzo cha ajali hiyo kikielezwa kuwa ni kufeli breki.

Kamanda wa Kikosi cha Usalama Barabarani, Wilbroad Mutafungwa, alikaririwa na chombo kimoja cha habari juzi akisema kuwa basi hilo lilikaguliwa Juni 13, mwaka huu, kwenye operesheni ya ukaguzi wa mabasi ya shule.

Mtafungwa alisema takwimu za ukaguzi uliofanyika kwa wiki mbili baada ya uzinduzi huo, zinaonyesha jumla ya mabasi 2,090 yalikaguliwa, kati yake 1,594 yalionekana mazima na 359 yalikutwa na matatizo madogo, 137 yalikuwa na matatizo makubwa na kung'olewa namba.

Akizungumzia maeneo hayo 12, Mhandisi Makule alisema, dereva yeyote kabla ya kuanza safari ni lazima afanye ukaguzi wa gari lake kwa kuhakikisha mifumo muhimu ya nje na ndani ya chombo chake ipo sawa kama alivyofundishwa.

"Kwa nje unaangalia kama tangi la mafuta halivuji na kwenye tairi lazima ulikague kama limetoboka au limekatwa, limefungwa vizuri, lina upepo wa kutosha, limekatwa au limelika halipaswi kwenda safari," alisema.

Alisema katika eneo la mbele la gari vitu ambavyo vinapaswa kuangaliwa ni wiper (kifuta maji), kioo na taa kama zinawaka au kufanya kazi.

"Visipofanya kazi mtu akaendesha gari akakutana na mvua tayari kiusalama sio sawa, kama anakanyaga breki taa haziwaki kwa maana hiyo hazimwonyeshi ishara wengine anaweza kupata ajali.

"Ukiingia ndani kuna kitu kinaitwa dashibodi (dash body) pale taa zote zinazoonyesha mifumo kama inafanya kazi vizuri, lazima awashe gari ahakikishe zinafanya kazi kama gari ina tatizo aweze kugundua kupitia taa hizi.


"Dereva huwa tunamwambia aziangalie hizo taa kuhakikisha wakati wote zinafanya kazi. Pia lazima ahakikishe mfumo wa usukani upo vizuri, huwa tunafundisha namna ya kukagua, anauchezesha kuhakikisha upo vizuri."



Kagua injini



Kagua tairi




Kagua Dash Bodi



Kagua maji



Kagua Oil

Pia alisema jambo lingine linalopaswa kukaguliwa ni breki za gari, dereva anatakiwa kuwasha gari lake kuangalia zinafanya kazi vizuri kama alivyofundishwa.

"Kama breki za gari hazifikii viwango kama alivyofundishwa, hilo gari linatakiwa kurekebishwa kabla ya kuanza safari," alisema na kuongeza:

"Lazima afungue eneo la injini, hii inatokana na aina ya gari, aangalie kama hakuna uvujaji wowote, hakuna mkanda uliolegea, je, hakuna kitu chochote kilichokaa ndivyo sivyo, ajihakikishie upande wa injini hakuna mlio wowote usio wa kawaida."

Alisema kama dereva akiwasha gari na kusikia mlio ambayo sio wa kawaida kwenye chombo chake, amefundishwa namna ya kuufuatilia.

Kama ni gari ya abiria, dereva anatakiwa kuhakikisha viti vimekaa vizuri pamoja na mikanda (ya abiria na wake) kama inafanya kazi, ili iwasaidie pindi inapotokea dharura wawapo safarini.

Akizungumzia ushiriki wao kama chuo kwenye suala la usalama barabarani mhandisi huyo alisema wamehakikisha wanakuwa na uhusiano na wadau likiwamo Jeshi la Polisi ambao wanafanya kazi nao kwa karibu kwa lengo la kuwapatia mafunzo.

"Tunashirikiana nao katika kuendesha mafunzo ya ukaguzi wa magari wale wanaokagua magari tunahusika kuwafundisha wakiwamo maofisa wa polisi, tunashirikiana nao kutoa elimu wakati wa wiki ya nenda kwa usalama barabarani.

"Vyama vya madereva tupo nao karibu, matokeo yetu tunayopitisha kuhusiana na madereva, wadau wanakuja tunayaangalia kwa pamoja kuangalia wapi pa kuboresha na matatizo, sehemu kubwa ni sehemu ya kufundisha," alisema.

Alisema wapo madereva wachache ambao hawatekelezaji majukumu yao ndiyo maana kuna sheria ndani ya Jeshi la Polisi.

"Ni kweli ajali zinazoongezeka kwa sababu baadhi ya wale ambao wamefundishwa hawafanyi majukumu yao au inachangiwa na wale ambao hawajafundishwa, hivi ni vitu vinatakiwa kuangaliwa vizuri, elimu bado inatakiwa kwa sababu wengi waliofundishwa wanafanya vizuri," alisema.

Alisema wito wao, wanahitaji nguvu ya wadau wengi kwenye sekta ya usafirishaji hasa katika eneo la utoaji wa elimu.

"Wananchi wamekuwa sehemu ya kuchangia ajali, wito wetu wawaache wataalamu wafanye kazi zao kitaalamu kama walivyofundishwa, unakuta gari la abiria mwananchi anachangia kwa kumwambia dereva achochee mwendo.

"Lakini, abiria hawa hawa wakiambiwa watoe taarifa hawataki kutoa ushirikiano kwa Jeshi la Polisi, kitu kinafanyika ndivyo sivyo hawatoi taarifa," alisema.

**TAKWIMU ZA AJALI**

Waziri wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Yussuf Masauni, akiwasilisha bungeni makadirio ya mapato na matumizi ya fedha kwa mwaka 2022/23 alisema, katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi 2022, jumla ya matukio makubwa ya ajali 1,594 ya usalama barabarani yaliripotiwa.

Alisema matukio hayo yaliripotiwa katika vituo vya polisi ikilinganishwa na 1,228 yaliyoripotiwa katika kipindi kama hicho mwaka wa fedha 2020/2021.

"Takwimu zinaonyesha kuwa matukio 366 ya usalama barabarani yameongezeka sawa na asilimia 29.8.

"Kati ya matukio hayo ya ajali, 874 yalisababisha watu 1,191 kupoteza maisha na 2,139 kujeruhiwa. Takwimu hizo zimeongezeka ikilinganishwa na matukio 756 ya ajali yaliyosababisha vifo vya watu 999 na majeruhi 1,589 katika kipindi kama hicho mwaka 2020/2021.

Alisema kwa ujumla ajali nyingi kati ya hizo zimesababishwa na madereva kutozingatia sheria za usalama barabarani, ubovu wa magari na miundombinu ya barabara.

HABARI KITAIFA

# Nyuki wazua taharuki shuleni wajeruhi walimu, wanafunzi

**Na Said Hamdani,** LINDI

KUNDI la nyuki ambalo halikujulikana limetokea wapi limezua taharuki baada ya kuvamia Shule ya Msingi ya Kamena Wilaya ya Liwale mkoani Lindi na kujeruhi walimu na wanafunzi.

Taarifa kutoka wilayani humo na kuthibitishwa na mmoja wa walimu wa shule hiyo, Rehema Mwaitenda, zinaeleza tukio hilo lilitokea saa nane mchana, Julai 26, mwaka huu.

Mwaitenda alisema siku ya tukio, yeye na walimu wenzake wakiwa wanaendelea na majukumu yao ya kikazi, kundi hilo la nyuki lilivamia shuleni hapo na kuwashambulia walimu na wanafunzi.

Alisema katika uvamizi huo, wanafunzi wanane pamoja na walimu wawili walikimbizwa Hospitali ya Wilaya mjini Liwale na kupatiwa matibabu baada ya kung'atwa na nyuki hao.

"Katika uvamizi ule wanafunzi wanne walilazimika kupumzishwa wodini kutokana na maumivu makali," alisema mwalimu huyo.

Mmoja wa wauguzi katika hospitali hiyo, ambaye hakupenda jina lake liandikwe gazetini kwa kuwa sio msemaji wa hospitali, alithibitisha kuwapokea majeruhi hao na kueleza kuwa walitibiwa na kuruhusiwa kurejea majumbani mwao, huku wanafunzi wanne wakalazimika kupumzishwa kwa muda.

"Ni kweli juzi tuliwapokea majeruhi wasiopungua kumi, wakiwamo walimu wawili na wanafunzi wanane," alisema.

Hata hivyo mmiliki wa shule hiyo hakupatikana kuzungumzia tatizo hilo na haikufahamika mara moja iwapo nyuki hao walitokea wapi.

Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo, Noel Manyasa, akizungumza na Nipashe alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kueleza kuwa wanafunzi wanaendelea vizuri.

"Tuliwaita watu wa maliasili wakawafukuza nyuki hao, lakini mti waliokuwa wametua kwa wingi tuliukata ili kutowavutia kurudi," alisema.

Aidha, alisema wanafunzi wanane na walimu wawili walijeruhiwa wakalazwa Hospitali ya Wilaya ya Liwale kwa matibabu zaidi na kwamba hali zao zinaendelea vizuri huku wanafunzi wanne wakipewa mapumziko.

# Jela miaka minane kwa kumuua mkewe

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

MAHAKAMA Kuu Tanzania Kanda ya Mwanza, imemhukumu Bahati Marko (45), kifungo cha miaka minane jela kwa kosa la kumuua mkewe, Esta Josefu kwa kumpiga mateke tumboni na kufariki dunia papo hapo.

Mwanamke huyo ameacha mtoto mchanga wa siku saba.

Kabla ya hukumu hiyo iliyotolewa na Jaji Mfawidhi wa Mahakama hiyo, John Kahyoza, Wakili wa Serikali, James Pallangio, akimsomea mshtakiwa maelezo ya kesi yake, alisema mwanaume huyo alimtaka mkewe aliyekuwa amejifungua kwenda kuishi kwa mama yake, lakini mke alikataa ndipo ugomvi upolizuka na kumpiga hadi kifo.

Wakili Pallangio alidai tukio hilo lilitokea Januari 28, mwaka 2020 na kwamba mshtakiwa na mke wake walikuwa wakiishi katika kijiji cha Shilabela/Lulembela, Wilaya ya Mbogwe, Mkoa wa Geita.

Alidai, baada ya mshtakiwa huyo kugundua kuwa mke wake amefariki aliondoka kwenda mgodini na kukaa hadi alipokamatwa na polisi na kupelekwa kituo cha Masumbwe, baada ya mahojiano alifikishwa mahakamani.

Baada ya maelezo ya awali, Jaji Kahyoza alimuuliza mshtakiwa huyo kama maelezo aliyosomewa na wakili yana ukweli.

Mshtakiwa huyo alijibu, "ni kweli nilimuua mke wangu bila kukusudia."

Jaji Kahyoza alimuuliza mshtakiwa alitumia nini kumuua mke wake na kujibu alitumia mikono yake kwa kumpiga mateke tumboni na ngumi sehemu mbalimbali za mwili wake na kufariki dunia papo hapo na kuondoka kwenda mgodini.

Kutokana na mshtakiwa kukiri kosa lake, Jaji Kahyoza alimsomea hukumu hiyo.

"Mahakama hii imekutia hatiani kwa kukiri kosa lako la kumuua mke wako bila kukusudia, pia mahakama hii inakutaka ujitetee ili iweze kukupunguzia adhabu."

Mshtakiwa huyo akitetewa na wakili wa kujitegemea Penina Mashimba, alidai kuwa mteja wake amejutia ndiyo maana amekiri kosa bila ya kulazimishwa.

Aidha, alidai mteja wake amekaa mahabusu miaka miwili na miezi sita na amejifunza na kuiomba mahakama hiyo kumpa adhabu ndogo ya kifungo cha nje.

Wakili Pallangio aliiomba mahakama hiyo kutoa adhabu kali dhidi ya mshtakiwa huyo kwa kuwa inaonyesha mshtakiwa huyo hakutumia busara katika kumwadhibu mkewe hasa sababu iliyotolewa na kwamba alikuwa na mfumo dume.

Alidai mtuhumiwa huyo hata baada ya kumpiga alimuacha na kuondoka kwenda mgodini hadi hapo polisi walipomkamata.

"Alimpiga mchana tena akiwa ana mtoto mchanga wa siku saba na kusababisha mtoto kukosa mapenzi ya mama yake, hivyo naomba mahakama hii itowe adhabu kali kwa mshtakiwa, ili iwe fundisho kwa wanaume wenye tabia ya kuwapiga wake zao," alisema.

Jaji Kahyoza alisema kosa alilolitenda mshtakiwa linastahili kifungo cha maisha, na kwamba tukio hilo ni la kikatili na kumhukumu jela miaka minane.

**"Mahakama hii imekutia hatiani kwa kukiri kosa lako la kumuua mke wako bila kukusudia, pia mahakama hii inakutaka ujitetee ili iweze kukupunguzia adhabu." Mshtakiwa huyo akitetewa na wakili wa kujitegemea Penina Mashimba, alidai kuwa mteja wake amejutia ndiyo maana amekiri kosa bila ya kulazimishwa.**


EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

**IMEDURIWA - OMBI LA KUONYESHA NIA: KUBUNI NA KUTEKELEZA MIRADI YA UWEKEZAJI WA KIJAMII KWA MAKABILA YALIYO PEMBEZONI YANAYOJITAMBUA KAMA WAZAWA ASILIA. KUMBUKUMBU NAMBA. 10007446**

EACOP Ltd, Kampuni ya Kimataifa ya Mafuta na Gesi, inaalika taasisi (kampuni au AZAKI) zenye weledi na uzoefu kuonesha nia ya kubuni na kutekeleza miradi ya uwekezaji wa kijamii kwa makabila yaliyo pembezoni yanayojitambua kama wazawa asilia yanayoguswa na Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP).

Mradi wa EACOP unahusisha ujenzi na uendeshaji wa bomba litakalofukiwa chini ya ardhi litakalovuka mipaka ya nchi mbili na litakalosafirisha mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka Pwani ya Mashariki ya Tanzania kwa ajili ya kusafirisha mafuta hayo kwenda katika masoko ya Kimataifa. Bomba hili litaanzia Kabaale katika wilaya ya Hoima nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoani Tanga nchini Tanzania. Urefu wa Bomba ni kilomita 1,443, kati ya hizo, kilomita 1,147 zitakuwa Tanzania.

**MAELEZO MAFUPI KUHUSU MAWANDA YA HUDUMA**

Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) unatafuta huduma kutoka kwa shirika lenye uzoefu wa kutosha (Kampuni au AZAKI zinaweza kuitikia ombi la kuonyesha nia) ili kubuni na kutekeleza mipango ya uwekezaji wa kijamii na kujenga uwezo kwa jamii za makabila takribani thelathini (30) yaliyo Pembezoni yanayojitambua kama wazawa asilia yanayoguswa na Mradi wa EACOP
Jamii hizi ziko katika mikoa ya Tabora, Manyara, Dodoma na Tanga.

Muundo wa programu utazingatia msaada kwa shughuli za kitamaduni (wafugaji au wawindaji) wa makundi haya ikijumuisha lakini sio tu usimamizi wa ardhi, afya ya mifugo na usimamizi, mahitaji maalum ya wanawake na inapaswa kuundwa kutumia mfumo wa pamoja unaozingatia mahitaji ya uhifadhi na uendelevu.

**VIGEZO MUHIMU VYA KUZINGATIA:**

Taasisi zitakazoonesha nia zinaalikwa kuambatanisha maombi yao pamoja na taarifa zifuatazo:

- Uthibitisho wa uzoefu katika kubuni na kutekeleza miradi ya uwekezaji wa kijamii kwa makabila yaliyo pembezoni yanayojitambua kama wazawa asilia.
- Uthibitisho wa usajili na leseni ya sasa ya biashara kwa makampuni au usajili wa Asasi zisizo za kiserikali (AZAKI kwa Asasi zisizo za kiserikali (AZAKI).
- Uthibitisho wa usajili wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA pamoja na cheti cha uthibitisho wa kulipa kodi kwa mwaka wa fedha uliopita.
- Ombi la usajili kwenye hifadhi data ya EWURA ya Watoa Huduma ya Ugavi wa Ndani (LSSP) na mrejesho wa wakat wa kuwasilisha nia unashauriwa sana kukusanywa.
- Kuzingatia kanuni za ushirikishaji wa wazawa za 2017 na ufafanuzi wa kampuni ya wazawa.
- Ubia kati ya makampuni/mashirika ya kitaifa na kimataifa unaruhusiwa.

Taasisi zenye nia ya kuleta maombi, uwezo na rasilimali za kutekeleza shughuli au kazi zilizoorodheshwa hapo juu zinapaswa kueleza nia yao pamoja na kuambatanisha nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe **procurement.tz@eacop.com** (ukubwa usizidi **20Mb**) saa au kabla ya saa tisa kamili saa za Afrika Mashariki (EAT) tarehe **7 August 2022.** Kichwa cha barua pepe kiwe **KUMBUKUMBU NAMBA. 10007446.**

Muhimu: Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na taasisi (kampuni au AZAKI) zitakazoonyesha nia ili kutengeneza orodha ya taasisi za awali zenye vigezo vinavyotakiwa. Taasisi zitakazokidhi vigezo tu ndiyo zitapokea na kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA) pamoja na mwaliko wa kuwasilisha zabuni katika kuendeleza mchakato wa zabuni.

Taarifa zote za kuonyesha nia zinapaswa kuandikwa kwa lugha ya Kiingereza.

216971202

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Bila utawala bora, hakuna klabu bora

**DHANA** ya utawala bora inahubiriwa dunia nzima. Nia ya injili hii ya utawala bora ni kuhakikisha kila kitu kinakwenda kwa mujibu wa taratibu. Na taratibu zikifuatwa maana yake ni kuwa kila kitu kitafanywa kwa uwazi.

Mpira wa miguu ni sehemu ya dunia hii tunayoishi. Ni mchezo ambao unahusisha wadau wengi, kutokana na ukweli kuwa mpira wa miguu ndiyo unaoongoza kwa kuwa na mashabiki wengi kuliko mchezo mwingine wowote.

Klabu za mpira wa miguu kama ilivyo vyama vya mpira wa miguu ni taasisi ambazo zinaongozwa kwa mujibu wa katiba ambazo zimeziunda ikiwamo kanuni za uendeshaji zinazotokana na katiba hizo na miongozo ya vyama vya mpira wa miguu vilivyo juu yao.

Ni katika utaratibu huo ndiyo maana umekuwapo mgawanyo wa majukumu. Klabu zina viongozi wa kuchaguliwa kwa mujibu wa katiba zilizoasisi taasisi hizo. Viongozi ndiyo wanaowajibika kwa mkutano mkuu wa wanachama.

Kwa mamlaka hayo ambayo uongozi umepewa na mkutano mkuu, una majukumu mbalimbali ya kutekeleza. Baadhi ya makujumu hayo ni kuajiri sekretarieti pamoja na mabenchi ya ufundi. Kocha mkuu kwa kawaida ndiye kiongozi wa Benchi la Ufundi.

Kwa mantiki hiyo sekretarieti inatarajiwa kuundwa na wataalamu kulingana na nafasi za kazi walizoomba kwa kuzingatia sifa zao.

Utaratibu huo huo ndiyo unaotumika vilevile kwa kuajiri Benchi la Ufundi kwa kuzingatia matakwa ya kocha ambaye ndiye anayeongoza benchi hilo likihusisha wataalamu wa nyanja nyingine za mpira wa miguu.

Hali ni mbaya, kwani sasa imekuwa kawaida kwa mwenyekiti au makamu mwenyekiti kufanya kazi za ofisa habari. Au mjumbe au mwanachama kufanya kazi za kocha (kusajili wachezaji).

Imefika mahali huwezi kujua nani ni katibu mkuu (mtendaji) katika klabu, na nani ni mwenyekiti au makamu mwenyekiti katika klabu au chama cha mpira wa miguu katika ngazi tofauti.

Nini kifanyike kama sekretarieti ina upungufu, udhaifu au ni mbovu? Kama ilivyo kwa mwajiri yeyote, kama mfanyakazi anashindwa kutekeleza majukumu yake kulingana na maelekezo aliyopewa anachukuliwa hatua za kinidhamu.

Katika utaratibu huo huo wa utawala bora, shughuli za mpira wa miguu hazitakiwi kuingiliwa na mamlaka nyingine nje ya uzio huo. Mfano, Shirikisho la Kimataifa la Mpira wa Miguu (FIFA) halitaki serikali kuingilia vyama vya mpira wa miguu.

Ingawa dhana hii imekuwa ikipotoshwa na baadhi ya viongozi dhaifu, ukweli ni kuwa FIFA inaamini katika utawala bora. Ni katika dhana ya utawala bora kila mwenye wajibu wake atatekeleza, kila mwenye haki yake ataipata.

Lakini hiyo itawezekana tu iwapo waliopewa majukumu/dhamana kulingana na katiba na miongozo mingine watatekeleza.


Kwa upande wa uchaguzi hiki ndicho kipindi chake ambapo kwa dhana ya utawala bora zimeundwa Kamati za Uchaguzi. Kamati hizi zinafanya kazi kwa mujibu wa Katiba ambazo ndizo msingi wa kuundwa kwao pamoja na kanuni za uchaguzi.

Katiba inaeleza sifa za uongozi (kwa maana ya watu wanaostahili kugombea, ingawa haki ya kuchagua inabaki kwa mpigakura). Kanuni kwa upande wake zinaelezea taratibu za uchaguzi (mchakato mzima) hadi viongozi wanapochaguliwa.

Au timu inashiriki katika mashindano X. Lakini kabla hujaingia katika mashindano ni lazima usome na ujue kanuni za mashindano husika, vinginevyo utakuwa msumbufu na kusababisha usumbufu kwa wadau wengine bila sababu za msingi.

Hayo yote ni matatizo ya kutozingatia utawala bora. Ni vizuri kuzingatia kanuni vinginevyo mtu anaweza kuonekana kituko mbele ya jamii/umma bila sababu za msingi. Huwezi kuwa na klabu bora huzingatii utawala bora.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Kocha Simba naye ameona kama yale yale



Na Adam Fungamwango

**MSIMU** uliopita Simba ilipoteza kila kitu, kuanzia ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Kombe la FA, lakini ilitolewa kwenye raundi ya kwanza tu ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Kilichosaidia kidogo na kutuliza hali ya hewa Simba ili kufanikiwa kutinga hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika kwa kuitoa Red Arrows ya Zambia na ikaenda hadi hatua ya robo fainali ya michuano hiyo, kabla ya kutolewa kwa mikwaju ya penalti dhidi ya Orlando Pirates ya Afrika Kusini.

Hiki ndicho angalau kilichowafanya mashabiki wa Simba watulie. Uchunguzi wangu mdogo umeonyesha kwa miaka ya karibuni, baada ya timu hiyo kufanya vema kwenye michuano ya kimataifa, wanachama na mashabiki wa Simba hufurahia zaidi timu yao kuwa kwenye hatua za makundi za michuano ya kimataifa kuliko hata ligi ya Tanzania.

Wanaona huko ndiko wanakostahili, na ndiyo maana wanapotolewa mapema kwenye michuano hiyo kama ilivyokuwa dhidi ya UD Songo ya Msumbiji miaka kadhaa iliyopita, wanasikitika sana na uongozi unakuwa uko lawamani.

Wanaona timu yao imeshakuwa kubwa ya kushindana kwenye mechi za kimataifa zaidi.

Baada ya kukosa kila kitu na kuishia hatua hiyo, wanachama na mashabiki wa klabu hiyo walitoa maoni kuwa baadhi ya wachezaji hawastahili tena kuichezea timu yao.

Wakasema ni kweli wameifanyia mema na makubwa, lakini kwa sasa hawana tena uwezo huo, hivyo wanahitaji wachezaji wengine wenye uwezo, vijana na wenye kupambania timu.

Wakasema wapo wachezaji ambao wana umri mkubwa, hivyo hawawezi tena kuleta kitu kipya.

Kuna wachezaji ambao wameshapata mataji na mafanikio, hivyo wanaona ni kitu cha kawaida. Hawafanyi tena jitihada, hivyo wanatakiwa wachezaji wengine ambao watakuja kusaka sifa zao binafsi huku ikitaka kutwaa mataji wakiwa na klabu yao.

Wanachama na mashabiki wa Simba wakawataja majina wachezaji ambao hawapaswi kuwamo kwenye klabu.

Inawezekana ni uzito wa viongozi wao, au kwa kuona labda wachezaji wanaotajwa kuwa waondoke bado wana mikataba, waliamua kuondoka nao na kwenda nchini Misri kwenye kambi ya kujiandaa na msimu mpya wa mashindano ya ndani na nje ya nchi.

Kuondoka kwao tu kulizua manung'uniko kwa baadhi ya wanachama na mashabiki wa klabu hiyo wakisema pamoja na kwamba wamesajili baadhi ya wachezaji wapya, lakini haikutakiwa tena kuwa na wachezaji hao.

Viongozi wakaja na kauli kuwa wanamwachia Kocha Mkuu Zoran Maki ili kuangalia nani anamhitaji na nani hamhitaji.

Kama ilikuwa ni kuogopa kuvunja mikataba, kuogopa lawama, kocha amekuja na kile kile ambacho wanachama na mashabiki wa Simba walikuwa wanakisema na kukihitaji.

Tayari kocha ameshatamka kuwa hahitaji kuwa na wachezaji Thadeo Lwanga raia wa Uganda, Meddie Kagere, Mnyarwanda na Mkongomani Chris Mugalu.

Unaweza ukadhani kuwa kocha huyo ambaye yuko nchini Misri alikaa kikao na mashabiki wa Simba Dar na kumweleza. Nao baadhi ya wachezaji waliotaka waondoke ni hao hao.

Tayari kuna taarifa kuwa straika mwingine wa Simba John Bocco yuko kwenye uangalizi, naye panga laweza kumpitia.

Pia taarifa kutoka jijini Ismailia iliko kambi ya timu hiyo ni kwamba kuna wachezaji wengine watatu ambao kocha haridhishwi nao na amewaweka mategoni, hivyo chochote kinaweza kutokea.

Hili ndilo viongozi wa Simba walilishindwa kulifanya tangu mwanzo. Hata hivyo wasilaumiwe sana kwa sababu walitaka kumpa uhuru kocha aamue.

Sasa kama ameamua na atazidi kuamua, viongozi wa klabu hiyo wanapaswa kukubali matakwa yake hata kama yatawagharibu kuvunja kibubu kwa sababu ndivyo walivyohitaji.

Kama si hivyo wangefanya hivyo wao mapema. Yoyote atakayemwona hafai, basi aondolewe bila kumwangalia aibu mtu asoni, na atakayetaka asajiliwe au nafasi zinazotakiwa kusajiliwa basi apatiwe haraka.

Inawezekana kwa sasa hatoeleweka kwa baadhi ya watu, lakini kocha huyo anaweza kuwa ni msingi mzuri wa Simba kurudi kwenye makali yake yaliyozoeleka kwa kusajili wachezaji wenye uwezo na ubora mkubwa wa kuipambania timu, badala ya baadhi ya wachezaji wanaocheza 'kifaza', kimazoea, na walioshuka viwango.



Kaimu Meneja Idara ya Uzalishaji wa kampuni ya Mbolea ya Yara Tanzania, Frank Lugoba ( kushoto ) akizungumza na wasambazaji wa kampuni hiyo wakati wakitembelea katika kiwanda cha Yara, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Wasambazaji hao kutoka maeneo mbalimbali nchini walikuja kushiriki mkutano wa mwaka wa kujadili jinsi ya kukuza ushirikiano kwa manufaa ya pande zote mbili. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wafurahia azimio haki ya mazingira

**Na Jenifer Gilla**

WADAU wa mazingira wamefurahishwa na uamuzi wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa (UN), kupitisha azimio la haki ya mazingira salama, wakieleza ni hatua muhimu kukabiliana na uchafuzi wa mazingira na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Utu na Mazingira (HUDEFO), Sarah Pima, alisema uamuzi wa baraza hilo uliotangazwa Julai 28, mwaka huu, utachochea nchi kuchukua hatua madhubuti na iliyoratibiwa kulinda mazingira.

"Sio jambo geni kwa sababu hii haki tayari ilipitishwa na baraza baada ya mashinikizo makubwa kutoka kwa watetezi wa mazingira. Lakini kitendo cha baraza kuu nalo kuidhinisha kumeongeza nguvu kwa mataifa kutilia mkazo suala hili na natumai tutapata matokeo mazuri," alisema Sarah.

Mkurugenzi wa Tanzania Cleanup and Conservation Initiative' (TCCI), Salum Kingungo, alisema kuwa kutambuliwa kwa haki hiyo kisheria kunawapa wanaharakati wa mazingira nguvu zaidi, ili kupinga sera na miradi inayoharibu ikolojia ili kutetea maisha ya viumbe hai.

"Hii ni habari njema kwetu kama wadau wa mazingira kwa kuwa inatupa nguvu ya kusimama mstari wa mbele kupinga mambo vitendo vyote vinavyoharibu mazingira kuanzia miradi hadi tabia binafsi za watu," alisema.

Wakati Mwenyekiti wa Asasi ya Kiraia ya Maendeleo Endelevu inayojishughulisha na uhifadhi wa mazingira (SDN), Freddy Kwezy, azimio hilo litazisukuma nchi kuweka haki ya mazingira yenye afya kwenye katiba za kitaifa na mikataba ya kikanda na kuhimiza mataifa kutekeleza sheria hizo.

Alisema japokuwa kuna sheria za kitaifa zilizoundwa kupunguza uchafuzi wa mazingira na kulinda viumbehai, lakini sheria hizo hazitekelezwi kikamilifu na zinapokiukwa wananchi wanashindwa kuiwajibisha serikali na kampuni husika.

"Kutangazwa azimio hilo kutaongeza kasi ya kupinga sera za uharibifu wa mazingira chini ya sheria ya haki za binadamu. Itasaidia watu kutetea haki yao ya kupumua hewa safi, chakula bora, mazingira yenye afya na yasiyo na sumu kufanya kazi, kusoma na kucheza," alisema.

Akizungumza baada ya kupitishwa azimio hilo, Mkurugenzi Mtendaji wa Mpango wa Mazingira wa Umoja wa Mataifa (UNEP), Inger Andersen, alisema kuwa azimio hilo linasaidia kutetea haki ya kupata hewa safi.

"Tumesubiri kwa muda mrefu kwa hili, lakini hii inaonyesha kwamba sasa kuna mshikamano na mabilioni ya watu ambao wanahisi uzito wa migogoro mitatu ya sayari, migogoro ya mabadiliko ya tabianchi, upotevu wa mazingira na uchafuzi wa mazingira," alisema.

Azimio hilo linafuatia baada ya Aprili, mwaka huu Baraza la Haki za Kibinadamu la Umoja wa Mataifa kutangaza upatikanaji wa mazingira safi, yenye afya na endelevu kuwa haki ya binadamu.

Wakati hayo yakiendelea nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara zinaelezwa kukabiliwa na matatizo makubwa ya kimazingira hali inayotishia uhai wa viumbe na maendeleo endelevu.

Kwa mujibu wa taarifa ya Benki ya Dunia (WB), mabadiliko ya hali ya hewa yaliyokithiri ni tishio kubwa kwa maendeleo ya nchi hizo ikiwamo ukame, mafuriko, mmomonyoko wa udongo, uharibifu wa ardhi oevu na ukatwaji wa miti.

Wakati Shirika la Umoja wa Mataifa la Mpango wa Mazingira linaonyesha kuwa zaidi ya asilimia 70 ya watu wanaoishi Kusini mwa Jangwa la Sahara wanategemea misitu kwa ajili ya maisha yao.

Aidha, Afrika inapoteza makadirio ya dola bilioni 195 kila mwaka za mtaji wake asilia kupitia mtiririko wa fedha haramu, uchimbaji madini haramu, ukataji miti ovyo, biashara haramu ya wanyamapori, uvuvi usiodhibitiwa na uharibifu wa mazingira na hasara.

UN inakadiria kuwa kifo kimoja kati ya sita cha mapema husababishwa na uchafuzi wa mazingira, na kwamba makumi ya mamilioni ya watu huhamishwa kila mwaka kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa huku upotevu wa viumbe hai ukitishia kuporomoka kwa mfumo mzima wa ikolojia.

# Vijiji 20 kupatiwa umeme wa uhakika

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imekubali kupokea mradi uliotelekezwa na Kampuni ya Madope Hydro Power Company Limited wilayani Ludewa, mkoani Njombe ili kuboresha upatikanaji wa umeme wa uhakika kwa wananchi wa vijiji 20 vya eneo hilo.

Kusambazwa kwa umeme kwenye vijiji hivyo kulikwamba kutokana na waya unaotumika kuwa mdogo ikilinganishwa na mahitaji ya wananchi wanaotumia nishati hiyo kwa shughuli za kiuchumi kama kuendesha mashine za kukamulia alizeti, kukoboa na kusaga nafaka.

Akiongea na wanakijiji wa Ludewa Mtaku jana, Waziri wa Nishati, January Makamba alisema, serikali kupitia TANESCO wamefanya mazungumzo na wahusika na kufikia makubaliano ambayo yatawezesha maboresho ya miundombinu muhimu.

"Kwa sasa katika megawati 1.7 zinazozalishwa, umeme unaotumika ni 0.3 na pia kampuni hii ya Madope itapata mapato ikiwa tutanunua umeme wote unaozalishwa na kuwapelekea wananchi," alisema Makamba.

Kadhalika, Waziri Makamba alisema, wataalamu wa TANESCO watafika Lugarawa Agosti 7, mwaka huu, ili kufanya tathmini ya miundombinu ya usafirishaji umeme pamoja na kusaini mikataba ya makubaliano na ifikapo Februari, 2023 wananchi wote wa Ludewa Mtaku wataanza kupata umeme wa uhakika.

Alisema pia watairuhusu TANESCO kukopa fedha benki kwa dhamana ya umeme watakaopata ili kuwasaidia wana Ludewa kupata nishati hiyo kwa uhakika.

"Kwa maana hiyo mpira upo kwa waendeshaji wa mradi kwa maana ya kanisa, diwani na halmashauri. Wakikubali hili ninalosema sasa, siku ya Agosti 7, wataalamu kutoka TANESCO makao makuu watakuwapo hapa Ludewa. Haya ni mambo ambayo tumeshajadiliana," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Madope, Mhandisi Kulwa Masanja, alisema mradi huo ulianza mwaka 2014 kwa ushirikiano kati ya Umoja wa Ulaya, Wakala wa Umeme Viijini (REA), Shirika la Maendeleo ya Viwanda la Umoja wa Mataifa (UNIDO), Jimbo Katoliki Njombe na kuratibiwa na Taasisi ya Acra Foundation.

Alisema mradi huo umewezesha utoaji wa huduma mbalimbali ikiwamo za afya katika Hospitali ya Mtakatibu Yohana Lugarawa, Kituo cha Afya cha Mlangali, zahanati 18, vyuo vya kati viwili, shule za sekondari tano na shule za msingi 19 na kituo cha kulelea watoto yatima.

Alisema mradi huo unakabiliwa na changamoto ya njia kuu ya kupitisha umeme kujengwa chini ya kiwango.

Masanja alisema pia kumekuwa na mfumo mbovu wa ukusanyaji wa mapato kutokana na mita walizoachiwa kuwa dhaifu na kwamba waliiomba TANESCO kukagua mradi kabla ya kuupokea ambao walibaini upungufu.

Aliiomba REA kuboresha miundombinu ya mradi huo huku wakiiomba TANESCO kuwachukua wateja wa vijiji hivyo, ili kampuni ibaki kuzalisha na kuuza umeme moja kwa moja bila kujihusisha na wateja.

Waziri Makamba alisema zinahitajika Shilingi bilioni sita kuboresha miundombinu na kuhakikisha upatikanaji wa umeme, huku akiahidi kuwa serikali itanunua nishati yote itakayozalishwa.

# Aweso azivunja Jumuiya za Watumia Maji

**Na Thobias Mwanakatwe,** MONDULI

WAZIRI wa Maji, Jumaa Aweso, ametangaza kuzivunja Jumuiya za Watumia Maji eneo la Mto wa Mbu wilayani Monduli, mkoani Arusha, baada ya wananchi kuzilalamikia hazifanyi kazi vizuri.

Alichukua uamuzi huo baada ya wananchi kuzuia msafara wake wakiwa na ndoo za maji, mabango na matawi ya miti wakitaka serikali itatue tatizo la maji. Wananchi hao walimweleza waziri kuwa kumekuwa na upendeleo wa ugawaji wa maji yanayopatikana kwa kuwagawia wafanyabiashara wenye hoteli (camp) huku wananchi wakitaabika bila maji. Walidai kuwa Kamati za Maji ndizo zinafanya kazi ya kupeleka maji kwa wafanyabiashara huku taasisi zikiwano shule zikinyimwa na kusababisha wanafunzi kushindwa kwenda kwenye vyoo.

Devota Martin, mjumbe wa Serikali ya Kijiji cha Kigongoni, alisema changamoto ya maji katika eneo la Mto wa Mbu linatokana na miundombinu ya maji kuwa midogo ambayo ilijengwa tangu mwaka 1970.

"Maji yanapelekwa kwa wenye fedha shule yetu Kigongoni hawaendi choo na hawapikiwi chakula kwasababu hakuna maji," alisema.

Waziri Aweso, akijibu malalamiko ya wananchi hao alisema serikali iliagiza Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), wayaainishe maeneo yote yenye changamoto.

Kutokana na hali hiyo alimtaka Meneja wa RUWASA Mkoa wa Arusha, Joseph Makaidi, atowe maelezo kwa wananchi kuhusu hatua zilizofikiwa mpaka sasa dhidi ya changamoto ya maji eneo la Mto wa Mbu.

Meneja wa RUWASA Mkoa wa Arusha, Makaidi alisema zaidi ya Sh. bilioni 1.7 zimetengwa kwa ajili ya kumaliza tatizo sugu la maji katika eneo helo. Alisema kinachosubiriwa kwa sasa ni kukamilisha taratibu za ununuzi na hatimaye aweze kutangazwa mzabuni atakayeanza kujenga mradi wa maji.

Naye Waziri wa Maji, Aweso alisema serikali iliwaagiza RUWASA kuainisha maeneo yote yenye changamoto ya maji ili yaweze kupatiwa ufumbuzi.

# IFM yatakiwa kuchapisha utafiti kimataifa

**Na James Kandoya**

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, amekitaka Chuo cha Usimamizi wa Fedha nchini (IFM), kuhakikisha machapisho ya utafiti wake yanachapishwa katika majarida ya kimataifa.

Katika hotuba yake iliyosomwa kwa niaba yake na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Amina Khami Shabani, kwenye uzinduzi rasmi wa Jubilei ya mika 50 ya chuo hicho iliyofanyika jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, alisema kwa kufanya hivyo kutaitangaza nchi na kujulikana.

Alisema kuwa chuo hicho kinapaswa pia kuja na mpango mkakati wa kuhakikisha kinaboresha mitaala yake ili kuzalisha wataalamu wanaoweza kushindana mahitaji ya soko la ajira.

Kwa mujibu wa Dk. Mwigulu, uamuzi wa kuchapisha machapisho ya utafiti wa chuo kwenye majarida ya kimataifa ni muhimu kwa kuwa utasaidia chuo hicho kufahamika katika medani mbalimbali nje na pia fursa kwa wanafunzi wake.

"Ni wakati muafaka kwenu kama taasisi kujikita kwenye kufanya tafiti ambazo mwisho wake zitachapishwa kwenye majarida mbalimbali ya kimataifa, ili kukitangaza chuo na nchi kwa ujumla," alisema.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Baraza la Chuo hicho, Prof. Godwin Mjema, alisema pamoja na mafanikio yaliyopatikana, chuo kinakabiliwa na uchache wa wahadhiri.

Alisema kuwa hadi sasa kuna wahadhiri 78 wa ngazi ya udhamivu na wengine wako kwenye hatua mbalimbali za masomo.

Naye Mkuu wa Chuo hicho, Dk. Emmanuel Mzava, alisema, hadi sasa jumla ya wahitimu 53,044 walimaliza chuoni hapo tangu kuanzishwa kwake.

Pia idadi ya kozi zimeongezeka na kufikia 33 mwaka huu kutoka kozi mbili za usimamizi wa fedha na bima kilipoanzishwa mwaka 1972.

Idadi ya machapisho imeongezeka kutoka 28 mpaka 84 na kuongeza kuwa katika kipindi cha miaka mitano iliyopita chuo kimefanya machapisho 332.



Mthamini kutoka Kampuni ya Trace Associates, Queen Lyakurwa, akichukua taarifa za mali zisizohamishika kwa ajili ya kuandaa taarifa ya ulipaji wa fidia ili kupisha mradi wa uchimbaji madini ya Nickel, utakaofanywa na kampuni ya Tembo Nickel wilayani Ngara. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wadau walia uhaba maabara za binadamu, wanyama

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

LICHA ya umuhimu wa bioteknolojia kwa masuala muhimu ya afya kwa binadamu na wanyama, vinywaji, chakula, viwanda na mazingira, sekta hiyo inakabiliwa na changamoto zinazoirudisha nyuma ikiwamo ukosefu wa maabara, wataalamu na ajira.

Mwasisi wa Bioteknolojia Tanzania, Prof. Paul Gwakisa, alisema hayo mjini hapo, katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), kwenye maadhimisho maalum ya siku ya bioteknolojia yaliyowakutanisha wadau mbalimbali wakiwamo watafiti, wataalamu na wanafunzi wa vyuo vikuu mbalimbali.

Prof. Gwakisa, alisema viwanda vingi vimekuwa na mtazamo usio wa kibaioteknolojia na kuwakosesha ajira vijana wanaohitimu kozi inayohusu masuala hayo.

Mkuu wa Idara ya Microbiology, Parasaikolojia na Bioteknolojia, SUA, Prof. Christopher Kasanga, alibainisha uwapo wa matumizi ndivyo sivyo ya sayansi na sheria ya kubadilisha uwezo wa wanyama katika kuzalisha au sheria ya kutengeneza dawa na chanjo mbalimbali, vinahitaji utaratibu na sheria ili pamoja na wataalamu hao kufahamu sayansi lazima wazingatie sheria na kutengeneza vitu vinavyohitajika na nchi kwa muda na sehemu maalumu.

Akimwakilisha Makamu Mkuu wa SUA katika maadhimisho hayo, Mkurugenzi wa shahada za juu, Utafiti, Uhawilishaji wa Teknolojia na Ushauri wa kitaalamu SUA, Prof. Esron Karimuribo, alisema kuwapo kwa wataalamu wanaotokana na vyuo vilivyoko ndani ya nchi ni jambo muhimu kwa kuwa tasnia hiyo kwa sasa inaibukia na ni muhimu katika maendeleo ya taifa.

Prof. Karimuribo alisema uwapo wao ni msaada kwenye uzalishaji wa dawa mbalimbali kwa ajili ya matibabu, kusaidia kutengeneza vitendanishi vinavyotumika kutambua magonjwa na mfano wa wazi ni karibuni kusaidia kwa haraka kutambua matumizi ya dawa baada ya kuibuka kwa ugonjwa wa UVIKO-19.

"Linapokuja suala la uzalishaji kunahitajika chakula cha kutosha, vimekuja vyakula vingi kwa kutumia teknolojia ya bioteknolojia, kwa upande wa mazingira inasaidia mambo ambayo yanaendana na usafi wa mazingira na SUA inaongoza katika tasnia hiyo ya bioteknolojia kwa kuwa na watafiti wabobezi ambao ni msaada katika kuendeleza fani hiyo," alisema Prof. Karimuribo.

Nao wanafunzi waliohudhuria maadhimisho hayo, akiwamo Martin Michael, mwanafunzi wa mwaka wa tatu wa shahada ya kwanza ya sayansi ya afya ya jamii na maabara ya sayansi SUA na Mercy Swai, licha ya kuishukuru SUA, ofisi ya makamu wa Rais Muungano na Mazingira na Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), kufanikisha siku hiyo iliyofanyika Tanzania kwa mara ya kwanza, walieleza kunufaika na mafunzo kwenye maadhimisho hayo.

Waliishauri serikali kuunda wizara na bodi maalum itakayokuwa na uwezo wa kusimamia kwa ukaribu zaidi taaluma ya bioteknolojia kutokana na umuhimu wake.

Kwa upande wake Michael, alishauri kutokana na faida anayoipata kupitia kozi anayoisomea, anaamini itasaidia jamii na taifa kwenye eneo lake nyanja mbalimbali hasa kwenye afya ya magonjwa yanayotoka kwa wanyama.

# Kampuni yazindua mradi wa nne uzalishaji gesi ukaa

**Na Mary Geofrey**

KAMPUNI ya kuzalisha gesi ya TOL Gases Limited, imezindua mradi wa nne wa gesi ya ukaa wenye thamani ya Sh. bilioni 13.65 utakaozalisha tani mbili kwa saa moja.

Mradi huo uliozinduliwa katika kijiji cha Ikama wilayani Rungwe, mkoani Mbeya, unatarajiwa kuanza kutumika Desemba mwaka huu na utadumu kwa miaka 20 utazalisha gesi hiyo kwa matumizi ya viwandani na katika huduma za afya.

Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, mkoani Mbeya, Dk. Vincent Anney, akizindua mradi huo mwishoni mwa wiki, aliipongeza kampuni ya TOL Gases kwa kuendelea kuwekeza na kuahidi kuendeleza ushirikiano.

"Kama kampuni ambayo imekuwa na mchango mkubwa katika sekta ya viwanda na afya, tutashirikiana kwa karibu na kampuni ili kuhakikisha kazi yake inaendelea kunufaisha jamii na nchi kwa ujumla," alisema Dk. Anney.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya TOL Gases Limited, Daniel Warungu, alisema hatua ya kuzindua mradi huo ni kupanua soko lake la ndani na nchi nyingine kama Zambia, Zimbabwe, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Malawi.

Warungu alisema gesi wanayozalisha itatumika kwenye viwanda na matibabu, katika uzalishaji wa vinywaji, usindikaji wa bidhaa za chakula na utengenezaji wa vifaa vya kuzima moto.

"Gesi ya ukaa inayozalishwa na kampuni ya TOL Gases Limited ina mchango mkubwa katika ukuaji wa uchumi wa viwanda na maendeleo ya nchi kwa ujumla. Uzinduzi wa mradi huu mpya ambao ni wa pili katika kijiji hiki cha Ikama, ni mwendelezo wa jitihada zetu za kuunga mkono dira ya serikali ya uchumi wa viwanda kupitia utengenezaji wa bidhaa za ndani," alisema.

Pia alisema kampuni hiyo inaendelea kuzalisha aina nyingine za gesi za viwanda na za hospitalini katika viwanda vyake vitatu vilivyoko Dar es Salaam, Mwanza na Mbeya.

Alisema kiwanda kipya cha Ikama kitaongeza maradufu uwezo wa kampuni wa kuzalisha gesi ya ukaa na kuhakikisha upatikanaji wa gesi hiyo.

"Tunatarajia ongezeko la Sh. bilioni 8.2 katika mapato ya mwezi ikiwa ni ongezeko la asilimia 42 ya mapato yatokanayo na gesi ya ukaa pekee, hii itakuza mchango wetu katika mapato ya serikali kupitia ulipaji wa kodi na tozo za huduma katika halmashauri ambazo kampuni yetu inafanya kazi," aliongeza.

# Aweso aagiza maofisa maji kuwafikia wananchi

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WAZIRI wa Maji, Jumaa Aweso, amewaagiza maofisa wa mabonde ya maji nchini, kuacha kukaa ofisini na kwenda kuwafuata wananchi waliko kuwapa elimu ya utunzaji vyanzo vya maji ili kupunguza migogoro.

Pia amemwagiza Meneja wa Wakala wa Maji Mjini na Vijijini (RUWASA) wilayani Monduli, Mhandisi Neville Msaki, kuchimba visima viwili katika Kata ya Mswakini na Meserani ili kusaidia wanafunzi watakaosoma kwenye shule hizo mbili zinazojengwa kupata majisafi na salama.

Agizo hilo limetolewa jana wilayani Monduli na Waziri Aweso, wakati wa uzinduzi wa mradi wa Uhifadhi na Utunzaji wa Chanzo cha Maji cha Ziwa Miwaleni, vijiji vya Mungere na Majengo Tarafa ya Makuyuni na Manyara.

"Maofisa bonde nawaagiza tokeni ofisini na acheni 'kuchezea' kompyuta, nendeni mkatoe elimu kwa wananchi ya kufanya shughuli za kilimo nje ya mita 60, ili msizalishe migogoro isiyo ya lazima," alisisitiza.

Alisema maofisa bonde wanaleta taharuki baadhi ya maeneo kwa kufyeka mazao ya wananchi, waliolima ndani ya bonde, wakati hawakutoa elimu kwa wananchi ya kulinda vyanzo vya maji.

"Acheni kukaa maofisini kuchezea kompyuta Januari hadi Desemba, huku mkiacha wananchi wakilima ndani ya bonde, halafu muda wa kuvuna ukifika mnafyeka mazao yao hapana, msilete taharuki kwa wananchi toeni elimu," alisisitiza. Kuhusu Shule za Sekondari Mswakini na Meserani, alisema serikali imetoa fedha za ujenzi wa shule hizo, lazima zipatiwe huduma ya maji ili wanafunzi wasome bila shida ya maji.

Alimwagiza Meneja wa RUWASA, kutoa Sh. milioni 136 kwa ajili ya uchimbaji wa visima viwili katika Shule za Sekondari za Meserani na Mswakini, ambazo awali hazikuwa na sekondari, ili kunufaisha wanafunzi na watoto watakaosoma hapo ikiwamo wananchi wa vijijini vya jirani.

Awali, Mkurugenzi wa Idara ya Rasilimali za Maji Wizara ya Maji, Dk. George Lugomela, alisema chanzo hicho kitahudumia wananchi zaidi ya 22,448 na wengi wao wamenufaika na kilimo na ufugaji kutokana na uwapo wa ziwa hilo.

"Hapa wananchi wanalima mboga, migomba, maharagwe, mahindi na mpunga, wengine kunywesha mifugo yao sababu maji ya ziwa hili yapo ya kutosha," alisema.

Aliishukuru wizara kwa kuruhusu Sh. milioni 315 kutoka Mfuko wa Maji wa Taifa, kutekeleza mradi huo ikiwamo kuainisha mipaka, usimikaji wa mabango na ujenzi wa miundombinu katika ziwa hilo.

Awali, Laigwanani Julius Mariki, aliishukuru serikali kwa kutenga nyanda za mifugo kwa wafugaji na utengaji wa nyanda hizo utawezesha jamii hiyo kufuga kisasa na kuheshimu wakulima ili kuepuka migogoro isiyo ya lazima baina yao.

Pia alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutafuta fedha nje ya nchi na kuimarisha mahusiano kwa ajili ya kuboresha huduma za wananchi.



Kaimu Mkuu wa Mkoa wa Mwanza ambaye ni Mkuu wa Wilaya ya Magu, Salum Khalii (kulia), akibadilishana mawazo na Mkurugenzi Mtendaji wa Bank Of Africa (BOA), Adam Mihayo, wakati wa ziara ya kikazi ya mkurugenzi huyo kwenye ofisi hiyo mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wakulima waondolewa hofu kutumia mbolea

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Mbolea ya Yara Tanzania, imewaondolea hofu wakulima nchini wa upatikanaji na bei ya bidhaa hiyo nchini, kwa kuwa wanayo ya kutosha.

Aidha, imetoa motisha kwa wasambazaji wa mbolea kwa mshindi wa kwanza kampuni ya Hapco Agrobusiness Sh. 58,879,954.84, huku Nasa Kilimo, wakishika nafasi ya pili na kuzawadiwa Sh. 52,674,275.28 na Mtewele Traders wakiibuka washindi wa tatu na kupata Sh. 27,321,514.80.

Mkurugenzi Mtendaji wa Yara Tanzania, Winstone Odhiambo, alibainisha hayo wakati wa mkutano wa mwaka wa wasambazaji mbolea wa kampuni hiyo jijini Dar es Salaam, kwa lengo la kuboresha uhusiano na kutafuta suluhu za changamoto zinazojitokeza kwenye kazi za kila siku.

Aliishukuru serikali kwa kuleta mpango wa ruzuku ya bei itakayowezesha upatikanaji wa mbolea hiyo kwa bei nafuu kwa wakulima.

Kuhusu uwekezaji wa kampuni, Odhiambo alisema kampuni ya Yara imewekeza Dola za Kimarekani milioni 40, na ina uwezo wa kuzalisha tani 500,000 za mbolea kwa mwaka.

"Yara Tanzania inawatoa hofu wakulima nchini kuendelea na shughuli za kilimo bila hofu ya upatikanaji wa mbolea, lakini ukiacha soko la Tanzania, tunazalisha mbolea kwa soko la Rwanda, Afrika Kusini na Kenya," alisema.

Akizungumzia usajili wa wakulima unaoendelea, Meneja wa Uagizaji na Uuzaji Nje wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Louis Kasera, alisema wakulima ambao ni walengwa wa mpango huo wa ruzuku ya Sh. bilioni 150 ya serikali wanapaswa kuunga mkono ili kuleta tija kwa waagizaji na wasambazaji.

Naye Meneja wa Kidigitali wa Yara, Deodath Mtei, aliwataka wakulima kuichangamkia huduma mpya ya AfricaConect inayowezesha wakulima kupata mikopo ya pembejeo za kilimo na viuatilifu kutoka kwa washirika wao kupitia Benki ya Equity.

"Tokea tumezindua Africa Connect jumla ya wakulima 50,176 wamejisajili kwa Kanda ya Kaskazini huku wakulima 510 wakipata mikopo, tuna lengo la kuwafikia wakulima 80,000 nchini kote," alibainisha. Bwanashamba mwandamizi mstaafu wa Yara, Maulidi Mkima, alisema mbolea inatengenezwa kwa viwango na kufuata kanuni za hali ya juu ambayo inahitajika kwa wakulima.

Naye Kaimu Meneja Idara ya Uzalishaji wa Yara Tanzania, Frank Lugoba, akizungumza na wasambazaji hao aliwataka wafuate taratibu zilizowekwa na kampuni kwa ufanisi wa biashara zao kutoka mbolea inapotoka kiwandani mpaka inapowafikia.

# Benki ya BoA yawajengea uwezo wafanyabiashara wadogo wadogo

**Na Mwandishi Wetu,** MWANZA

BENKI ya Afrika (BOA) Tanzania, imewakutanisha wafanyabiashara wa kati na wadogo (SME) na kuwapatia ujuzi na maarifa muhimu kwa ukuaji mzuri na thabiti wa biashara zao.

Mafunzo hayo yalifanyika mwishoni mwa wiki ili kuwajengea uwezo kuhusu masuala ya kifedha, ikiwamo mbinu za utunzaji fedha, namna ya kukuza mtaji na kushirikiana ili kukua pamoja kibiashara.

Akifungua warsha hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa BoA, Adam Mihayo, aliwahimiza wajasiriamali na wafanyabiashara nchini kuchangamkia huduma za kifedha zinazotolewa na benki hiyo ili kuongeza tija.

"Sisi BoA, katika mpango mkakati wa miaka mitatu ni kuchangia katika ukuaji wa uchumi wa nchi. Sekta ya wafanyabiashara wadogo na wakati ni sekta muhimu na nyeti katika uchumi wetu inachangia asilimia 30 ya pato la taifa," alisema na kuongeza:

"Ukiangalia takwimu katika biashara 10, tisa zitatokea kwa wafanyabiashara wadogo na wa kati. Nawakaribisha Bank of Africa kwa kuwa ndiyo benki yenye mtazamo chanya unaolenga kuwasaidia wajasiriamali wadogo na wakati."

Aidha, alisema benki hiyo ilitoa mikopo kwa wajasiriamali wadogo na wa kati ya Sh. bilioni 32 mwaka jana, huku hadi Juni mwaka huu, walitoa Sh. bilioni 23, wakiwa na malengo ya kutoa zaidi.

"Katika mpango mkakati wa miaka mitatu pia tumepanga kutoa mikopo ya Sh. bilioni 132 kwa sekta hii nyeti na tunaamini katika kufanya hivyo tunachangia ukuaji wa uchumu wetu," alisema.

"Dhumuni kubwa la warsha hii ni kuwawezesha wafanyabiashara wa jijini Mwanza ambao ni wateja wetu katika maeneo mbalimbali, utafiti unaonyesha kwamba biashara nyingi hazifanikiwi kwa wafanyabiashara wadogo na wa kati ni kutotunza kumbukumbu vizuri, wanapata changamoto ya hesabu zao."

Baadhi ya wafanyabiashara waliohudhuria warsha hiyo, wameipongeza benki hiyo kwa kuinua biashara zao, huku wakiomba kuboreshwa zaidi kwa huduma zilizoko.

Mkuu wa Kitengo cha Wateja Wadogo na Kati wa BoA, Ninael Mndeme, aliwahakikishia wafanyabiashara hao kuwa huduma za mikopo zitatolewa wakati wote kwenye benki kwa kuzingatia taratibu na sheria.

# Wizara kushindanisha waandishi vitabu vya riwaya

**Na Elizabeth Zaya**

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, amesema wizara hiyo imeandaa programu maalum ya kushindanisha waandishi wa vitabu vya riwaya ili kutoa motisha na kuhamasisha uandishi.

Alisema hayo mwishoni mwa wiki kwenye mkutano na wahariri wa vyombo vya habari kuhusu kipaumbele na maeneo ya kimkakati utekelezaji kwa mwaka 2022/23 na kuendeleza ushirikiano pamoja na utambulisho wa miradi inayosimamiwa na wizara hiyo.

Prof. Mkenda alisema lengo la mashindano hayo ni kuhamasisha uandishi wa sanaa ya kina wa vitabu hivyo, ambavyo vitauzwa na kujipatia kipato huku wakiendelea kujitangaza ndani na nje ya nchi.

"Kuna mambo mazuri yanayoendelea sasa ambayo hayajaandikwa na endapo yakiandikwa yatakuwa yanatoa funzo kubwa kwa wananchi, kwa hiyo tumeanzisha programu hii ili kuhamasisha waandishi wa vitabu," alisema Prof. Mkenda.

"Kuna fungu ambalo limetengwa kwa ajili ya mashindano haya, lengo kubwa tunataka haya mambo mazuri yanayotokea kwenye mazingira yetu, nchini kwetu yaandikwe kwa kina na kwa kuzingatia sanaa ya hali ya juu."


Pia vitabu vitakavyoandikwa vizuri vitapelekwa kutumika shuleni.

"Hatusemi kwamba vile vitabu vilivyoko sasa havitatumika tena, hapana, isipokuwa tunataka viandikwe na vitu vingine tena ambavyo vinaelezea mazingira mazuri ya sasa ambayo wengi hawayajui," alisema Prof. Mkenda.

"Wengi wetu hapa shuleni tulisoma vitabu vya riwaya ambavyo vimesimuliwa kwa ustadi na vinavutia kuendelea kusoma, kwa hiyo kama ambavyo tulifurahia kusoma vile vingine, tunataka tena viandikwe na vingine, lengo ni kutaka waandishi waandike kwa kina mazuri yanayotokea na yaliyoko katika mazingira ya sasa."

"Kwa hiyo hii ni fursa nyingine kwa waandishi wa vitabu nchini kuichangamkia na tunaamini kupitia programu hii, itahamasisha zaidi uandishi wa vitabu."

Kwa mujibu wa Prof. Mkenda, ipo fursa duniani ya vitabu kutafsiriwa katika lugha mbalimbali, ambayo itamwingizia kipato mwandishi, kuitangaza kazi yake na nchi kwa ujumla.




Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Dk. Rashid Mohamed Chuachua, akipokea hundi ya Sh. milioni 60 kutoka kwa Meneja wa Benki ya NMB Kanda Nyanda za Juu, Straton Chilongola, akimwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, ikiwa ni mchango wa kuwezesha maonyesho ya Nanenane yanayofanyika kitaifa mkoani Mbeya mwaka huu 2022. Benki ya NMB ni mmoja ya wadhamini wakuu wa maonyesho hayo ya Nanenane. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# DIT, TGNP waingia makubaliano kiteknolojia

**Na Grace Gurisha**

TAASISI ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT), imeingia makubaliano na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) ya kuanzisha na kuendesha programu ya pamoja ya kitovu cha teknolojia, jinsia na uvumbuzi.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Mkurugenzi Mtendaji wa TGNP, Lilian Liundi, baada ya kusaini makubaliano hayo ya miaka mitatu, jijini Dar es Salaam.

Alisema mkataba huo unalenga kutengeneza vumbuzi na bunifu za kiteknolojia zenye lengo la kutatua changamoto za kijinsia, ili kurahisisha uwezeshaji wa wanawake na usawa wa kijinsia.

"Teknolojia imekuja na fursa nyingi za maendeleo, lakini wanawake wengi hawayafikii maendeleo haya kutokana na sababu mbalimbali ndiyo maana tukaja na makubaliano haya," alifafanua Liundi.

Alisema takwimu za Umoja wa Mawasiliano ya Kimataifa za mwaka 2019 zinaonesha kuwa kuna pengo la kijinsia kwa asilimia 10 katika matumizi ya mtandao (internet) duniani, ukanda wa Jangwa la Sahara ni wa pili kwa kuwa na pengo kubwa la kijinsia kwa matumizi ya mtandao huo.

Alisema kwa upande wa Tanzania takwimu hizo, zinaonesha kuwapo kwa pengo la kijinsia kwa asilimia 11, wanawake watumiaji wa mtandao ni asilimia 77 na wanaume asilimia 86, hali hiyo imesababisha mafanikio ya wanaume yamejulikana zaidi kuliko wanawake.

Kwa upande wake, Makamu Mkuu wa Chuo cha DIT, Prof. Preksedis Ndomba, alisema uandaaji bunifu hizo unawezekana kwa kuwa taasisi zote malengo yake yanafanana.

Alisema DIT ni taasisi inayotambulika ndani na nje ya Tanzania kama iliyobobea katika TEHAMA inayozingatia masuala ya jinsia katika taratibu zake, ikiwamo aina ya kazi za kiteknolojia zinazotengenezwa na wanafunzi.

"DIT itaendelea kuwa kiongozi wa kutatua changamoto mbalimbali kwenye jamii kwa kutumia TEHAMA, lengo ni kuendelea kutambulika Afrika na ulimwenguni," alibainisha Prof. Ndomba.

Alisema taasisi hiyo imebuni teknolojia nyingi ikiwamo atamizi ya mtoto njiti, teknolojia ya kumsaidia mtoto kupumua na mifumo ya kuweka taarifa ili kutatua changamoto zinazowakabili wananchi hususan waishio vijijini.

Alisema ili kufikia usawa wa kijinsia, wameandaa mwongozo wa kuwashirikisha wanawake katika shughuli mbalimbali zinazofanywa chuoni hapa ili kukuza sayansi na teknolojia.

Nipashe
Spotika



NYOTA WANAOWEZA KUWA WAFUNGAJI BORA EPL UK. 12-13




# NYOTA WENYE DENI ULAYA MSIMU HUU

LUKAKU

## ISIKUPITE

SHIRIKISHO la soka barani Ulaya, UEFA, linachunguza tukio la mashabiki wa klabu ya Fenerbahçe kuliimba jina la Rais wa Russia, Vladimir Putin wakati wa kipigo cha mabao 2-1 kutoka kwa Dynamo Kiev ya Ukraine wakati wa mchezo wa kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya. Nyimbo hizo zilisikika katika Uwanja wa Fenerbahçe mjini Istanbul muda mfupi baada ya Vitaliy Buyalskiy kuifungia Dynamo bao la utangulizi katika mchezo ambao klabu hiyo ya Ukraine ilisonga mbele katika muda wa ziada.



**LONDON,** England

PAUL Pogba aliondoka Manchester United msimu huu wa joto, akisema alitaka kuonyesha klabu hiyo 'ilifanya makosa'.

Kiungo huyo wa kati wa Ufaransa, ambaye amejiunga na Juventus kwa uhamisho wa bure, alinyanyua Kombe la Dunia akiwa na taifa lake mwaka 2018, lakini alishinda tu taji la Ligi ya Europa na Kombe la Carabao katika ngazi ya klabu katika kipindi chake cha pili cha miaka sita pale kwenye dimba la Old Trafford.

Kampeni zake tatu za mwisho zilizaa mabao nane pekee. Lakini Pogba ni moja ya jina kubwa katika Ligi Kuu tano bora barani Ulaya mwenye pointi ya kuthibitisha msimu huu.

Kutoka kwa wachezaji ambao walikuwa na msimu mbaya wa mkopo hadi kwa wengine ambao hawajacheza, ni nani mwingine anayehitaji msimu mzuri zaidi. Hebu tuwaangalie hawa:

### Dele Alli

Kiwango cha Dele Alli kimepungua kwa kiasi kikubwa katika miaka minne iliyopita.

Misimu yake mitatu ya kwanza pale Tottenham Hotspur akiwa kijana na katika miaka yake ya mapema alifunga mabao 46. Lakini badala ya kusonga mbele, alionekana kurudi nyuma, akifunga mabao 21 tu katika kipindi cha miaka mitatu na nusu kiasi ambacho Spurs walimruhusu kwenda Everton bila malipo yoyote ya awali.

Mabadiliko ya mandhari hayakumsaidia sana Alli, hata hivyo na alishindwa kufunga katika mechi yoyote kati ya 11 alizocheza, akiwa na mwanzo mmoja pekee katika nusu msimu.

Huku presha ikishuka Everton baada ya kukwepa kushuka daraja, je, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 anaweza kwenda vyema kwa kikosi cha Frank Lampard mwaka huu? Na ni nani anayejua kitakachofuata kwa mchezaji huyo wa mara moja wa kimataifa wa England ikiwa hatafanya hivyo?

### Donny van de Beek

Ni vigumu kufikiria uteuzi bora wa usimamizi kwa wakati bora zaidi kwa Donny van de Beek kuliko kuwasili kwa Erik ten Hag kule Manchester United.

Kiungo huyo wa kati Mholanzi alicheza chini ya Ten Hag mara 110 akiwa Ajax, akifunga mabao 32, kabla ya kuondoka kwenda United.

Lakini alianza mechi nne tu za Ligi Kuu England ndani ya takriban mwaka mmoja na nusu chini ya Ole Gunnar Solskjaer kabla ya kwenda kwa mkopo Everton. Pengine angetarajiwa kuondoka Old Trafford msimu huu wa joto, lakini chini ya Ten Hag, ana nafasi kubwa ya kuwa sehemu muhimu ya timu na kuthibitisha kuwa Solskjaer alikosea.

### Romelu Lukaku

Nafasi ya pili ya Romleu Lukaku pale Chelsea ilikuwa ya kukatisha tamaa.

Mshambuliaji huyo wa Ubelgiji alijiunga tena na Chelsea kutoka Inter Milan kwa pauni milioni 97.5 msimu uliopita.

Ni wazi hakuwa na furaha pale Stamford Bridge na ingawa alifunga mabao 15, kulikuwa na hisia kwamba, Chelsea hakuichezea kwa uwezo wake na alikuwa ametoka nje ya timu kabisa.

Sasa amerejea Inter kwa mkopo na ingawa lilikuwa chaguo lake kuondoka, atataka kumwonyesha kocha Thomas Tuchel kile angekuwa nacho kama angeunda timu karibu naye.

### Marcus Rashford

Marcus Rashford anaweza kufanya makubwa kwa Manchester United ili kuwaonyesha makosa wale wanaodai kuwa kazi yake ya nje ya uwanja imeathiri soka lake.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 24 aligonga vichwa vya habari mwaka 2020 na jukumu lake katika kushawishi serikali kutoa vocha za chakula cha shule bila malipo kwa wanafunzi katika likizo za kiangazi.

Alishinda kitabu bora cha mwaka katika Tuzo za Vitabu za Uingereza mwaka huu za 'You Are A Champion', ambazo ziliandikwa ili kuwatia moyo vijana.

Lakini Rashford alifanikiwa kufunga mabao matano pekee katika michuano yote msimu uliopita hakuna hata moja tangu Januari.

Rashford lazima aanze vyema msimu huu ikiwa ataonyesha kuwa anafaa kuwa sehemu ya kikosi cha England kitakachoshiriki michuano ya Kombe la Dunia nchini Qatar.

### Dean Henderson

Golikipa wa wa Manchester United, Dean Henderson ni mwingine ambaye ana takriban miezi mitatu ya kujithibitishia ubora ili acheze katika kikosi cha England cha Kombe la Dunia baada ya kujiunga na Nottingham Forest kwa mkopo.

Mwishoni mwa msimu wa 2020-21, alionekana kumpita David de Gea na kuwa kipa chaguo la kwanza la United - na alitwa katika kikosi cha England cha Euro 2020, ingawa alilazimika kujiondoa kutokana na jeraha.

Hiyo ilikuja baada ya misimu mitatu kamili ya soka wakati wa muda wa mkopo na Shrewsbury na Sheffield United. Lakini msimu uliopita hakucheza hata mechi moja ya Ligi Kuu.

### Jesse Lingard

Jesse Lingard atakuwa na hamu ya kuwaonyesha Manchester United walipaswa kumpa nafasi zaidi msimu uliopita.

Maisha ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29 yalionekana kudorora hadi alipojiunga na West Ham kwa mkopo miezi 18 iliyopita. Alifunga mabao tisa katika mechi 16 na akashinda mchezaji na bao bora la mwezi Aprili 2021.

Alirejea Old Trafford kwa kujiamini sana msimu uliopita wa joto na alifunga mara mbili akitokea benchi mnamo Septemba, lakini alianza mechi nne pekee msimu mzima katika mashindano yote.

Aliondoka Old Trafford mwishoni mwa mkataba wake na sasa amejiunga na Nottingham Forest ambako ana nafasi ya kuonesha ubora wake.

## Extra Time

# NYOTA WANAOWEZA KUWA WAFUNGAJI BORA EPL

**LONDON,** England

MSIMU wa Ligi Kuu England 2022-23 ulifunguliwa rasmi Jumamosi kwa mechi ya Ngao ya Hisani kati ya Manchester City (mabingwa wa ligi) na Liverpool washindi wa pili.

**Na sasa mwishoni mwa wiki hii pazia rasmi la Ligi Kuu litafunguliwa na kuna washambuliaji wengi wanaotabiriwa kuweza kuibuka wafungaji bora msimu huu.**

Mohamed Salah wa Liverpool na Heung-Min Son wa Tottenham walishiriki Kiatu cha Dhahabu msimu uliopita, wakifunga mabao 23 kila mmoja.

Wakati huo huo, Cristiano Ronaldo wa Manchester United na Harry Kane wa Spurs ni miongoni mwa washindi wengine wa zamani wa tuzo hiyo wanaotarajiwa kutinga tena msimu huu.

Pia kuna wagombea wapya wanaowania tuzo hiyo, huku nyota wa Manchester City Erling Haaland na Darwin Nunez wa Liverpool wakitarajiwa kuanza msimu wao wa kwanza katika soka la Uingereza.

Makala hii inawaangalia nyota wanaoweza kuibuka kuwa vinara wa mabao msimu huu:

### Erling Haaland

Huenda bado hajapiga mpira kwenye Ligi Kuu England, lakini ni ngumu kuangalia zaidi ya Haaland anayeongoza kwenye orodha ya wafungaji msimu huu.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 alifunga mabao 86 katika mechi 89 alizoichezea klabu ya awali ya Borussia Dortmund na ilimchukua dakika 12 tu kufunga bao lake la kwanza akiwa amevalia jezi ya City huku akifunga bao katika ushindi wao wa kabla ya msimu mpya dhidi ya Bayern Munich.

Mzaliwa huyo wa Jiji la Leeds mwenye urefu wa futi 6 na inchi 5, hatakuwa na shida kuzoea ugumu wa mpira wa miguu wa Uingereza na ana uhakika wa kupata nafasi nyingi.

City wamekuwa wafungaji bora wa kitengo hicho katika kila misimu mitano iliyopita, ambayo ni pamoja na kufumania nyavu 99 msimu uliopita licha ya kutokuwa na mshambuliaji wa kati anayetambulika katika kikosi chao.

Haaland atakuwa kiongozi na dalili zote zinaonyesha kwamba anaweza kufunga mabao 20 zaidi angalau kwenye ligi msimu huu.

City watatumaini atatinga hatua kwa hatua watakapokabiliana na safari ngumu dhidi ya West Ham siku ya ufunguzi, wakiwa hawajashinda mechi yoyote kati ya tatu zilizopita kwenye Uwanja wa London.

### Harry Kane

Baada ya kuanza kwa taratibu msimu uliopita, Kane alimaliza kampeni akiwa amefunga mabao 17, ikiwa ni jumla yake ya chini kabisa katika Ligi Kuu tangu mwaka 2014.

Alifunga mabao sita pungufu kuliko mchezaji mwenzake Son na atatamani kurejea kileleni mwa chati msimu huu huku akitazamia kunyakua kiatu cha dhahabu cha nne kwenye Ligi Kuu.

Nahodha huyo wa England hapaswi kukosa huduma huku Son na Dejan Kulusevski, pamoja na wachezaji wapya waliosajiliwa, Ivan Perisic na Richarlison, watafanya kazi pamoja naye katika tatu ya mwisho.

Spurs pia wanapigiwa upatu kuwa na msimu mzuri chini ya Antonio Conte na ikiwa wanataka kuwapa changamoto Manchester City na Liverpool kileleni mwa msimamo, bila shaka Kane atalazimika kufunga zaidi.

Amehusika katika mabao 17 katika mechi 13 za Ligi Kuu dhidi ya Southampton (mabao 11, pasi za mabao sita).



HARRY KANE

### Gabriel Jesus

Gabriel Jesus ameondoka Manchester City na kwenda Arsenal na inaonekana wazi kuwa atacheza kama mshambuliaji namba moja pale kwenye Uwanja wa Emirates na atapata muda wa mara kwa mara wa kucheza.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 25 alifikisha idadi mara mbili pekee ya mabao ya Ligi Kuu ya England katika misimu sita akiwa na City.

Lakini kwa kiasi kikubwa alikuwa na jukumu la usaidizi kule Manchester, wakati anaweza kuwa mtu anayeongoza Arsenal.

Kocha wa washikabunduki hao, Mikel Arteta atatumaini kwamba Jesus anaweza kufunga mabao yatakayowawezesha kutinga hatua ya nne-bora na anaonekana kuwa chaguo zuri.

Washikaji hao wa London Kaskazini watakuwa na motisha ya ziada msimu huu.

### Callum Wilson

Mshambuliaji wa Newcastle United, Callum Wilson anatarajiwa kuwa na changamoto kubwa zaidi kwenye jedwali kufuatia kumalizika kwa msimu uliopita.

Wilson ni mfungaji aliyethibitishwa katika kiwango cha Ligi Kuu huku wakiwa bado hawajasajili mshambuliaji mwingine msimu huu wa joto, anaweza kutegemewa sana kufunga mabao - mradi ataendelea kuwa fiti.

Atakuwa na matumaini ya kupata mashuti mengi, huku Newcastle wakiwakaribisha Nottingham Forest waliopanda daraja katika mchezo wao wa ufunguzi. Vijana wa Eddie Howe wameshinda mechi tano kati ya sita za mwisho kwenye uwanja wa nyumbani.

### Mohamed Salah

Ni vigumu kumpuuza Mohamed Salah - na Liverpool wakikabiliana na Fulham kuanza msimu wao, kuna kila nafasi Mmisri huyo kupata mikwaju mingi inayolenga lango.

Mchezaji mwenzake Nunez pia atakuwa na matumaini ya kuanza kwa haraka baada ya kufumania nyavu mara nne katika mechi za kujiandaa.

## Nukuu

“KWENYE soka huwezi kujua, siwezi kusema kimsingi, yote inategemea. Lakini kimsingi, naweza kusema kuna uwezekano mkubwa akabaki na naweza kusema kama rais nitafanya kila niwezalo kwa ajili yake, atabaki Barcelona. Kitu cha kwanza kusema tunataka Frenkie de Jong abaki Barcelona. Tunampenda mchezaji huyu na yeye kama binadamu. Nataka abaki Barcelona. Ni mchezaji wa hali ya juu na mtu mzuri.” **Rais wa Barcelona, Joan Laporta.**



“KATIKA soka huwezi kujenga kitu muhimu ndani ya siku moja, unatakiwa kwenda hatua kwa hatua na kujaribu kuongeza ubora, kuongeza idadi ya wachezaji kwenye kikosi chako. Usisahau kuwa timu inapokaa kwenye nafasi nne za juu na kucheza michezo ya Ulaya unahitaji kukabiliana na mashindano manne kwa njia bora zaidi.” **Kocha wa Tottenhma Hotspur, Antonio Conte.**



“NAJIVUNIA kuvaa tena jezi hii ya Nacional. Asante kwa msaada wako wote. Tutaonana hivi karibuni namna gani tunaweza kuisaidia klabu kusonga mbele na mimi pia kuwa sehemu ya mafanikio yake.” **Luis Suarez.**





Beki wa kulia wa Yanga, Djuma Shaaban, akijaribu kuwalamba chenga wachezaji wa Zanaco kwenye mechi ya tamasha la Wiki ya Mwananchi lililofanyika mwaka jana. Jumamosi ijayo Yanga itakuwa na kilele cha wiki hiyo kwa mwaka huu. **PICHA: MAKTABA**

# YANGA ITAKAVYOFUNIKA WIKI YA MWANANCHI

**Na Adam Fungamwango**

JUMAMOSI ijayo, klabu ya Yanga inakwenda kukamilisha tamasha lake la kila mwaka ambalo limepewa jina la 'Wiki ya Mwananchi.'

**Ingawa bado mpaka sasa klabu hiyo haijatoa taarifa rasmi lakini tetesi zinasema kuwa huenda ikacheza mechi dhidi ya Vipers ya Uganda, au Red Arrows ya Zambia kwenye kilele cha tamasha hilo.**

Kuanzia leo tarehe moja Agosti, wanachama na mashabiki wa Yanga Tanzania nzima watakuwa kwenye pilikapilika ya kutembelea maeneo mbalimbali na kufanya shughuli za kijamii, ikiwa ni pamoja na kutoa misaada.

Wiki hii hutumika kutembelea vituo vya watoto yatima, hospitalini, magereza mbalimbali na maeneo mengine yenye uhitaji.

Mara nyingi klabu hiyo hufanya hivyo katika kile kinachoonekana kurudisha kwa jamii, kwani ni moja kati ya klabu mbili zenye mashabiki wengi nchini. Jinsi mashabiki wanavyojaa uwanjani kila inapocheza, kuifuatilia na kuishabikia, klabu hiyo imeona nayo ina cha kufanya kwa jamii hiyo.

Rais wa Klabu hiyo, Injinia Hersi Said ambaye amechaguliwa hivi karibuni anasema mwaka huu wamepania kuifanya Wiki ya Mwananchi kuwa ya kipekee.

Mwisho wa wanachama na mashabiki wa klabu hiyo kufanya yote hayo, yatahitimishwa Jumamosi wakati itakapocheza mechi ya kirafiki na mara nyingi huwa na timu kutoka nje ya nchi, kuashiria kufungua mwanzo wa msimu mpya.

Kabla ya mechi hiyo huwa kuna utambulisho wa wachezaji wanaotumika kwa msimu mzima wa mashindano.

Yanga iliamua kuifuata klabu ya Simba ambayo ndiyo mwanzilishi wa tukio kama hilo tangu 2009, ambayo mwaka huu italifanya kwa mara ya 13.

Aliyekuwa Mwenyekiti wa Simba wakati huo, Hassan Dalali ndiye aliyeasisi tamasha walilolíita Simba Day, akiwa na Katibu Mkuu wake Mwina Kaduguda na baada ya kuonekana kufana na kuwa na tija kila miaka inavyozidi kusonga mbele, watani zao nao wakaamua kuungana nao, mwaka 2019.

Ni tamasha ambalo huwa ni kama mtoko kwa familia, kwani licha ya soka, hujumuisha muziki na burudani zingine mbalimbali ambapo huanza mapema tu kuanzia sasa sita mchana na kuendelea.

Kuingia kwa Yanga nao kufanya tamasha lao kama ilivyokuwa kwa Simba kumezidi kuleta chachu kwani mchuano unakuwa haupo tu kwenye soka, bali hata kwenye kuangalia tamasha lipi limefana zaidi.

Hiyo inasababisha viongozi wa klabu hizo kuwa makini, ikiwamo ubunifu ili kufanya matamasha yao yavutie.

Mwaka huu Yanga inakwenda kufanya tamasha la Wiki ya Mwananchi kwa mara ya nne.

Mwandishi wa makala hii anakuletea matokeo ya mechi ambazo Yanga imecheza mechi zake hizo tangu ilipoanza mwaka 2019.

**1. Yanga 1-1 Kariobangi Sharks (2019)**

Ilikuwa ni Agosti 4, 2019, Yanga ilipomaliza Wiki ya Mwananchi yake ya kwanza kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam ikicheza dhidi ya Kariobangi Sharks kutoka nchini Kenya.

Hata hivyo, mashabiki na wanachama wa klabu hiyo hawakuwa na mwanzo mzuri, baada ya kulazimishwa sare ya bao 1-1 na kurudi nyumbani wanyonge.

Dakika tatu baada ya mapumziko, wageni walipata bao la kuongoza lililowekwa wavuni na Patrick Otieno.

Dakika tisa baadaye, yaani dakika ya 57 kwa mkwaju wa penalti. Alikuwa ni kiungo mpya aliyesajiliwa kutoka nchini Rwnada, Patrick Sibomana, aliyeikwamisha penalti hiyo wavuni na kuifanya mechi hiyo kwenda sare.

**2. Yanga 2-0 Aigle Noir (2020)**

Mwaka uliofuata ulikuwa mzuri kwa Yanga. Pamoja na kuliboresha vema tamasha lake, lakini ilipata ushindi wa kwanza kwenye mechi yake iliyocheza Agosti 30, 2020 kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa dhidi ya Aigle Noir kutoka Burundi.

Ni mechi ambayo ilimtambulisha kipa Erick Johora aliyekuwa akiidakia timu hiyo, wengi wakidhani kuwa ni Mrundi, lakini baadaye ilikuja kufahamika kuwa ni Mtanzania.

Msimu mmoja baadaye Yanga ilimsajili na mpaka leo bado yupo. Kwenye mechi hiyo alifanya kazi kubwa sana kuokoa mashambulizi ya wenyeji kiasi cha kuvutiwa naye.

Yanga ilishinda mabao 2-0, Tuisila Kisinda raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo akiwa ndiyo kwanza amejiunga na timu hiyo kutoka AS Vita Club akifunga bao dakika ya 38, kabla ya Mghana Michael Sarpong kupachika bao la pili dakika ya 51 kutokana na krosi ya Ditram Nchimbi.

**3. Yanga 1-2 Zanaco (2021)**

Mwaka jana, Yanga ilitia fora kwenye tamasha lake kwa kujaza watu wengi zaidi kuliko miaka iliyotangulia na kuvunja rekodi.

Hata hivyo, ndiyo mechi ambayo kwa mara ya kwanza ilipoteza kwenye kilele cha Wiki ya Mwananchi, ilifungwa mabao 2-0 dhidi ya Zanaco kutoka nchini Zambia.

Kwenye mechi hiyo iliyochezwa Agosti 29, Yanga ilianza kutangulia kwa bao la dakika ya 30, mfungaji akiwa ni Heritier Makambo akipata pasi safi kutoka kwa Feisal Salum.

Zanaco ilicharuka na kusawazisha dakika ya 60 kupitia kwa Ackim Mumba, kabla ya Kelvin Kapumbu kukwamisha mpira wavuni dakika ya 76, akiandikisha bao la ushindi kwa wageni.

## JE, WAJUA?



MASHABIKI wa Manchester United wamegawanyika kuhusu uteuzi wa Sir Alex Ferguson kuwa mshauri wa klabu hiyo. Kupitia Twitter mashabiki hao wanadai ni hatua nzuri, lakini sio wakati sahihi kwa mkongwe huyo kuingia kwenye bodi ya maamuzi wakati mambo mengi hayako sawa.



# Dodoma kuwa na mabasi makubwa ya abiria

**Na Augusta Njoji,**

DODOMA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini (LATRA), imekamilisha mpango mkakati wa usafiri ndani ya Jiji la Dodoma, unaolenga kuwa na mabasi makubwa kama ilivyo kwa Jiji la Dar es Salaam.

Mkurugenzi wa Udhibiti Usafiri wa Barabara kutoka LATRA, Johanses Kahatano, alieleza hayo mwishoni mwa wiki jijini hapo alipokuwa akijibu swali la mwandishi wa habari aliyehoji mkakati wa mamlaka hiyo kuimarisha usafiri Dodoma kutokana na kukua kwa kasi.

Alisema baada ya kukamilisha mpango mkakati wataalika wawekezaji.

"Kwa Dodoma tuna mpango mkubwa ambao ni kwa ajili ya kupata mabasi makubwa kama Dar es Salaam, pia mpango kazi wa usafiri Dodoma umekamilika baada ya hapo tutatoa fursa kwa wawekezaji wa kuweka viwango vikubwa. Kwahiyo Dodoma tupo na tunafuatilia. Pia Mpango kwa ajili ya usafiri," alisema.

Awali, Mkurugenzi Mkuu wa LATRA, Habibu Suluo, alisema kwa mwaka 2022/23, LATRA imejipanga kuhakikisha kuwa huduma bora na salama za usafiri ardhini zinawafikia wananchi, kuondoa kero mbalimbali.

Alisema kwa mwaka huo, Mamlaka imepanga kukusanya Sh. bilioni 41.7 kupitia vyanzo vyake vya mapato mbalimbali ikiwamo matumizi ya mfumo wa tiketi mtandao.

Pia LATRA imesajili kwenye kanzidata yake madereva 10,324 katika vyombo vya usafiri vinavyotoa huduma za usafiri wa kibiashara.



Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Maziwa ya Dodoma Halisi, Anthony Msanga, akizungumza na waandishi wa habari (hawapo pichani) jijini Dodoma juzi, kuhusu umuhimu wa wataalamu wa mifugo kutoa elimu kwa wafugaji ili waweze kufuga kisasa. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Mizengo Pinda atahadharisha w'biashara uchakachuaji bidhaa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda, amewataka wafanyabiashara nchini kuwa waadilifu na kujiepusha na kuchakachua bidhaa kwa kuwa inachangia kushusha ubora.

Aidha, alisema viongozi wa serikali wana wajibu wa kuwajibika kusaidia wafanyabiashara na wajasiriamali ili wafanye vizuri kwenye shughuli zao.

Alitoa kauli hiyo jana kwenye kongamano la uongozi na biashara lililoandaliwa na Taasisi ya Kingdom Leadership Network Tanzania (KLNT).

Alisema kuna wafanyabiashara kwa tamaa zao za kujipatia fedha kwa urahisi hukosa uadilifu na kuchakachua bidhaa hali inayosababisha kukosa ubora na kuharibu soko.

"Uadilifu katika biashara ni muhimu na kujiepusha kuchakachua bidhaa ili kupata fedha kwa urahisi, pia tunakutegemea uchangie serikalini ulipe kodi na ushuru unaotakiwa wewe ndiyo wa kwanza kukwepa, halafu unasema mimi mjasiriamali mzuri wewe sio mzuri," alisema. Alisema viongozi wa ovyo ndani chama au serikali wanatokana na kukosa misingi ya uongozi.

"Utawala unasimamiwa na serikali na katika mfumo wetu ulivyo serikali inawekwa pale, lakini inatokana na siasa, kwa hiyo katika kuongoza nchi, vyama uongozi lazima utambulike kwamba una nafasi kubwa sana, ukipata majitu ya ovyo kwenye chama, au serikali hamuendi, kwasababu hawana misingi ya uongozi, kila eneo utakalogusa uongozi ni lazima," alisema.

Kuhusu viongozi wa serikali kuwasaidia wajasiriamali, Pinda alisema, "Sisi ndiyo tumewaweka mtuongoze, ni lazima ukitoka hapa useme nitafanya juu na chini kuwasaidia wajasiriamali wadogo wafanye vizuri kwenye shughuli zao, kama hujali wewe siyo kiongozi mzuri."

Pinda ambaye ni mlezi wa taasisi hiyo, alisema uongozi ndiyo utakaomsaidia mjasiriamali kutoa mchango kwa taifa.

"Uongozi unaweza ukawa wa kuwekwa au kusimikwa, kwenye biashara tunazofanya kuna kitu hatufanyi, mtu anaanza kienyeji tu kama Mzee Pinda kuna misingi yake, wewe mjasiriamali ambaye una kampuni usipopata maarifa ya kukuwezesha kuwa kiongozi mzuri kwenye kampuni yako utafeli," alisema.

Kwa upande wake, Katibu Mkuu Kiongozi mstaafu, Balozi Ombeni Sefue, akizungumzia uongozi unaofaa katika dunia inayobadilika, alipongeza taasisi hiyo kwa kuandaa programu za kujenga vijana na wajasiriamali kwenye misingi ya uadilifu na ujasiriamali.

"Haitoshi kila mtu kulalamika hakuna ajira na hakuna wa kutengeneza ajira, nchi haiwezi kwenda mbali, lakini lazima kuwapa vijana ujuzi wanaohitaji ili kuanzisha biashara vizuri inavyopaswa na sio kukurupuka, kile unachotaka kufanya kipime kwa vigezo," alisema.

Hata hivyo, alisema kero zilizoko duniani ikiwamo ugonjwa wa corona na mfumuko wa bei unatokana na kutokuwa na uongozi mzuri.

"Mabadiliko ya hali ya hewa mwaka huu dunia inafanya mkutano wa 27 wa kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa (COP27) nchini Uswisi, lakini licha ya kufanyika kwake viongozi wamekuwa wakitoa ahadi zisizotekelezeka na nchi maskini zinaathirika zaidi japo wao sio walioharibu mazingira," alisema.

Awali Meya wa Jiji la Dodoma, Prof. Davis Mwamfupe, alisema katika mabadiliko ya kidunia lazima kuwe na viongozi ambao wameandaliwa vyema. "Mkutano huu unalenga kusisitiza katika hali ya kubadilika lazima uwaandae viongozi na maandalizi ya hao viongozi iwe wajasiriamali, kuna umuhimu wa kuandaa viongozi wafuate zile kanuni za msingi katika utawala, watende haki wawe na uwazi," alisema.

# Warajis wakumbushwa maamuzi kimkakati

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

TUME ya Maendeleo ya Ushirika imewataka Warajis Wasaidizi wa Vyama vya Ushirika katika mikoa nchini kuandaa mipango na kufanya maamuzi ya kimkakati yanayotekelezeka kwenye majukumu yao.

Kaimu Mrajis wa Vyama vya Ushirika, Juma Mokili, ambaye ni Mkurugenzi wa Utafiti na Mafunzo kutoka tume hiyo, alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki alipokuwa akifungua mafunzo ya menejimenti ya vihatarishi kwa warajis hao.

Alisema ili kupanga mipango inayotekelezeka katika tume hiyo ni lazima kuhakikisha wanazuia kila viashiria vihatarishi katika mipango yao. "Kama mnavyofahamu tuko hapa kwa ajili ya kuhudhuria mafunzo ambayo yatatujengea uelewa na kutuwezesha kuanzisha na kusimamia mifumo ya menejimenti ya vihatarishi katika ofisi zetu," alisema Mokili.

"Mafunzo haya yanafanyika kwa mujibu wa maelekezo yaliyomo kwenye mwongozo wa kuanza fremu ya menejmenti ya vihatarishi katika taasisi za serikali uliotolewa mwaka 2012 na Wizara ya Fedha na Mipango kupitia Idara ya Mkaguzi wa ndani."

Alisema lengo la mwongozo huo ilikuwa ni kutoa dira ya uanzishwaji na utekelezaji wa mfumo menejmenti ya vihatarishi katika taasisi za serikali. Awali, Mkaguzi Mkuu wa ndani wa serikali msaidizi wa vihatarishi, mifumo na udhibiti wa ndani, Abraham Msechu, alisema usimamizi wa vihatarishi ni eneo muhimu kwa kila taasisi katika utendaji kazi wake ili kufikia malengo waliyojiwekea.

Alisema hapo mwanzo walikuwa wanafanya kazi kwa kufikirika na kusababisha kutofikia malengo wanayojiwekea, lakini baada ya kuanza kutumia mfumo huo kumekuwa na mabadiliko makubwa.

Mkaguzi Mkuu wa ndani wa tume hiyo, Mwanaidi Kalela, alisema mafunzo hayo ni muhimu katika dhana ya vihatarishi, sifa na namna ya kuibua katika maeneo yao ya kazi.





## Wazazi waonywa kutumia watoto maonyesho Nanenane

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya, limetangaza msako na kuwachukulia hatua kali za kisheria, wazazi na walezi wale watakaowatumia watoto kwenye biashara zao wakati wa maonesho ya wakulima Nanenane yanayoanza leo.

Mwakilishi wa Kamanda wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Mbeya ambaye ni Ofisa wa Polisi Jamii, ACP Ndimbweku Mwalukasa, alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki wakati wa kutoa elimu kwa wananchi mambo wanayotakiwa kuyafanya kwenye maadhimisho hayo ambayo kitaifa yanafanyika jijini hapo.

Alisema miongoni mwa mambo wanayopaswa kuzingatia wananchi ni kuacha kuwatumia watoto kwenye biashara zao zikiwamo za kutembeza bidhaa mbalimbali kwenye maonyesho hayo na watakaobainika watashughulikiwa kwa mujibu wa sheria.

Aliwakumbusha wazazi na walezi usalama wa watoto wao wakati wa msimu huo wa maonyesho hayo kuhakikisha wanapotoka na watoto wawe makini ili wasipotee au kupata madhara mengine.

"Polisi jamii Mkoa wa Mbeya tumeamua kutoa elimu kwa wananchi juu ya masuala mbalimbali ikiwamo usalama na mali zao ili kujiepusha na madhara mbalimbali ikiwamo wizi na uhalifu mwingine," alisema.

Kwa upande wake, Ofisa wa Polisi Jamii Halmashauri ya Jiji la Mbeya, Vitalis Nyenza, alisema Jeshi la Polisi limejipanga kikamilifu kudhibiti vitendo vyote vya uhalifu kwa kuhakikisha doria na misako mbalimbali inaendelea kufanyika maeneo mbalimbali.

Aliiomba jamii kutoa ushirikiano ili kudhibiti na kubaini mahali penye viashiria vya vitendo viovu.

Kwa upande wake, Ofisa wa Kikosi cha Usalama Barabarani jijini Mbeya, Andreas Chale, alisema wamejipanga kusimamia sheria mbalimbali za barabarani.

Alisema miongoni mwa mambo watakayofanya kwenye maadhimisho hayo ni watumiaji wa vyombo vya moto kutumia njia zilizoainishwa na kuheshimu alama za barabarani ili kutowabugudhi watembea kwa miguu na watu wenye ulemavu.

Alielekeza madereva bajaji na bodaboda kutozidisha abiria na atayebainika kukiuka utaratibu atakamatwa na kuchukuliwa sheria.

# Wenye ulemavu hatarini magonjwa ya kuambukizwa

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WATU wenye ulemavu, wako hatarini kupata magonjwa ya kuambukizwa kutokana na kundi hilo kusahaulika licha ya serikali kuonyesha jitihada za kulishirikisha kwenye kampeni na elimu ya magonjwa hayo.

Kauli hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki na Mkuu wa Huduma za Tiba, Uongozi na Uchunguzi kutoka Hospitali ya Rufani ya Kanda Mbeya (MZRH), Dk. Uwesu Mchepange, alipozungumza na Nipashe kuhusu ushiriki wa watu wenye ulemavu kwenye maadhimisho ya Siku ya Homa ya Ini Duniani.

Dk. Mchepange alisema kwenye maadhimisho ya Siku ya Ini mwaka huu walijikita kulisaidia kundi la watu wenye ulemavu, ambalo kwa kiwango kikubwa halina elimu ya kutosha juu ya mapambano dhidi ya ugonjwa huo na kuwa kwenye hatari kubwa ya kuambukizwa au kuambukiza ugonjwa huo.

Alidai kuwa katika takwimu za mwaka 2021 duniani zaidi ya watu milioni moja wanapoteza maisha kila mwaka kutokana na homa ya ini duniani au vitu ambavyo vinavyoambatana na homa hiyo.

Alisema inakadiriwa asilimia 4.4 ya Watanzania, wanamaambukizi ya virusi vya homa ya ini, lakini watu wanaogopa zaidi virusi vya ukimwi kuliko virusi vya homa hiyo.

"Hatari ya ugonjwa wa ini inatokana na uwezo wa kuambukiza virusi vyake kuwa mkubwa zaidi kuliko virusi vya ukimwi ndiyo sababu ya kuliona kundi hili watu wenye ulemavu kulipa kipaumbele kwa sababu unapozungumzia homa ya ini hasa hii inayosabishwa na virusi inaambukiza kwa njia mbalimbali na njia kuu ni zile zile ambazo zinaambukiza virusi vya Ukimwi," alieleza Dk. Mchepange.

Alishauri jamii kuachana na ngono zembe na kutahadharisha kuwa ugonjwa huo hauna kinga na huambukiza pia kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto, kuchangia vitu vyenye ncha kwa wale wanajidunga dawa ya kulevya. Kwa upande wake, Daktari bingwa wa magonjwa ya ndani, Dk. Peter Kishimbo, alisema magonjwa ya homa ya ini dalili zake ni macho kuwa ya njano, homa, tumbo kuuma upande wa kulia, viungo kuuma, kuharisha na kutapika.

Mwenyekiti wa Chama cha Watu wenye ulemavu Mkoa wa Mbeya, Juma Mwampepo, aliushukuru uongozi wa Hospitali ya Rufani ya Kanda Mbeya kwa kutambua umuhimu wa kundi la watu wenye ulemavu ili kupata elimu ya homa hiyo kwa kuwa wengi hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu ugonjwa huo.

Aidha, Mwampepo alisema hospitali hiyo imeweka utaratibu kuwahudumia watu wenye ulemavu.

Aliziomba taasisi na idara nyingine kutumia utaratibu huo ili kusaidia watu wenye ulemavu kusikilizwa na kuhudumiwa kikamilifu bila vikwazo vyovyote.



Mwakilishi wa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya ambaye ni Ofisa wa Polisi Jamii, ACP Ndimbwelu Mwalukasa, mwishoni mwa wiki alitoa elimu ya usalama wa raia na mali zao katika maadhimisho ya Siku ya Wakulima maarufu Nanenane ambayo kitaifa yatafanyika jijini Mbeya. Jeshi la Polisi lilitoa elimu hiyo maeneo mbalimbali yenye mkusanyiko mkubwa wa watu. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Operesheni yanasa raia 169 wa kigeni kuingia nchini bila kibali

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

JESHI la Polisi mkoani Mbeya, limefanikiwa kuwakamata raia 169 wa kigeni kwa kosa la kuingia nchini bila kibali baada ya kufanya operesheni na misako mbalimbali katika kipindi cha kuanzia Januari hadi Julai mwaka huu.

Kwa mujibu wa taarifa ya Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, kati yao ni raia kutoka nchini Ethiopia (97), Somalia (37), Burundi (7), Rwanda (21), Kenya (2), Uganda (1), Malawi (1) na Angola (1).

Alisema miongoni mwa waliokamatwa ni watoto ambao waliokuwa wanasafirishwa kwenda nchi zingine kufanya kazi.

Aidha, Kamanda Matei alisema magari 11 yalikamatwa yakihusika kufanya biashara hiyo haramu ya kuuza watu.

Alitoa takwimu hizo ikiwa ni maadhimisho ya siku ya kupinga biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu, ambayo huadhimishwa kila mwaka Julai 30, kwa lengo la kutoa elimu na tathmini ya biashara haramu za watu.

Katika taarifa yake Kamanda Matei alisema, Watanzania saba walikamatwa kwa kosa la kujihusisha na biashara hiyo na kuwataja waliokamatwa kuwa ni Angelile Nasson (43), Brown Larisa (46), Augustino Michael (40), Hemed Abeid (46), Maneno Kujokwa (27), Paul Mwamkonga (47) na Kurwa Ngoro (35).

"Usafirishaji haramu wa binadamu ni kitendo haramu kwa sababu kimekatazwa na sheria za kimataifa hususani zile ambazo zinazotetea na kulinda haki za binadamu, sheria yetu ya kuzuia na kupambana na uhalifu wa aina hii "The Anti-Trafficking in Persons Act, No. 6, 2008 imeharamisha matendo yote yenye viashiria vya usafirishaji wa binadamu wenye lengo la kumtumikisha binadamu kwa kiunyonyaji na ikiwa ni pamoja na kumtendea matendo yanayokiuka haki zake kama binadamu," alisema Matei.

Kamanda Matei alieleza chanzo cha biashara hiyo kuwa ni mahitaji makubwa ya nguvu kazi ambayo sio ya gharama na inayopatikana bila kufuata sheria na taratibu zilizowekwa na serikali.

Aidha, kuibuka kwa soko la ngono katika baadhi ya nchi duniani ambalo linahitaji wanawake na wasichana uhitaji wa soko la viungo vya binadamu duniani kama figo. Vile vile viungo vya binadamu vinahitajika katika ushirikina.

Alisema mwaka 2021, kulikuwapo na tukio la kuwahusisha watoto 14 waliokolewa na Jeshi la Polisi Mkoa wa Mbeya wakiwa wanaenda kutumikishwa kazi ya kuchunga mifugo huko Wilaya ya Mbarali.

Kadhalika, hatua mbalimbali zilizofanywa na jeshi hilo kuwa ni kuwakamata na kuwachukulia hatua za kisheria wote wanaojihusisha na biashara hii, kuongeza juhudi za kuelimisha jamii ili ipate uelewa wa madhira wanayoyakuta wanawake, wasichana, watoto na vijana waodanganywa kwenda kufanya kazi ndani au nje ya nchi bila kufuata taratibu za kisheria.

Kufanya ukaguzi na utambuzi wa waathirika katika maeneo ya viwanja vya ndege na kutoa mafunzo maalum ya kuzuia na kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu.

Mafunzo ambayo yalihusisha maofisa kutoka ofisi ya katibu wa Sekretarieti ya Kuzuia na Kupambana na Usafirishaji Haramu wa Binadamu - Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Shirika la Tanzania Relief Initiatives, maofisa kutoka Jeshi la Polisi, Magereza na Uhamiaji, Idara ya Mahakama na Ustawi wa Jamii kwa lengo la kuwajengea uwezo na weledi katika utendaji kazi.

Alitoa wito kwa wananchi kuendelea kutoa taarifa za kuwafichua mawakala wa usafirishaji wahamiaji haramu kutokana na wengi wao kuwa ni wakazi wa maeneo yao na wanawajua na kuendelea kutoa taarifa wanapoona watu au kikundi cha watu wanachokitilia shaka ili hatua za haraka zinafanyike ikiwamo ya kuwakamata kwa ajili ya upelelezi na kujiridhisha juu ya uraia wao.





# PM aagiza wizara za habari kuhamasisha sensa

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa ameziktaka Wizara za Habari Zanzibar na Bara, kutumia vyombo vya habari kuelimisha jamii ili ifahamu maswali ya msingi yanayoulizwa kwenye sensa ya watu na makazi itakayofanyika Agosti 23, mwaka huu.

Majaliwa ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Kitaifa ya Sensa ya Watu na Makazi aliyasema hayo katika kikao cha sita cha kamati hiyo kilichofanyika mjini Unguja.

Alisema ili wananchi wajitokeze kuhesabiwa ni lazima wawe na taarifa watakayohojiwa kuondoa hofu ya maswali yanayoulizwa na upotoshaji.

Pia alisema ni muhimu kutumia mitandao ya kijamii kufikisha elimu hiyo kwa kuwa watu wengi wamo humo na taarifa zinawafikia kwa urahisi, huku akipongeza ushirikiano wa pande zote za Muungano.

Alimshukuru Mwakilishi wa Shirika la Umoja wa Mataifa linalosimamia Idadi ya Watu Duniani (UNFPA) nchini, kwa kuendelea kuunga mkono sensa huku akimhakikishia ushirikiano thabiti.

Mwenyekiti mwenza wa Kamati hiyo, Hemed Suleiman Abdulla, aliwashukuru viongozi wa kitaifa kwa kazi ya kuhamasisha wananchi kushiriki sensa.

Hemed ambaye ni Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, alizishukuru taasisi za dini na makundi mbalimbali kwa kuendelea kutumia fursa walizonazo katika kuwahamasisha walio kwenye dhamana zao.

Kwa upande wake mtakwimu mkuu wa serikali ya Zanzibar, Salum Kassim Ali, alisema makarani na wasimamizi wa sensa wameshapatikana na mafunzo yanaendelea kwenye shehia na kata.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati Kuu ya Kitaifa ya Sensa ya Watu na Makazi akifungua kikao cha sita cha kamati hiyo kilichofanyika Melia Hotel Mkoa wa Kaskazini Unguja. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Sababu kikwazo ukuaji kilimo mboga zatajwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKURUGENZI wa Idara ya Kilimo, Muhamed Khamis Rashid, amesema baadhi ya sera na sheria zinaathiri utekelezaji wa kilimo cha mboga na matunda, Zanzibar.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kikao cha kamati ya ushauri wa uzalishaji na uendeshaji wa kilimo cha viungo, mboga na matunda visiwani humo, alisema alipitia sera na sheria hizo na kubaini changamoto hiyo inayotakiwa kutatuliwa.

Kamati hiyo ilikutana Mjini Zanzibar kujadili maendeleo na changamoto za mradi wa viungo, mboga na matunda.

Alibainisha kuwa kuna sera nane zenye upungufu zinazoathiri kilimo hicho na masoko ikiwamo Sera ya Kilimo Zanzibar ya mwaka 2002 ambayo haikutoa kipaumbele kwa kilimo cha mboga na matunda.

Alisema sheria na sera hizo zitakapofanyiwa marekebisho zitaondoa changamoto zinazokwamisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo, ili kuhakikisha maendeleo ya kilimo ni makubwa na yenye tija.

Alibainisha kuwa mkakati wa uendelezaji wa kilimo cha mboga na matunda pamoja na kilimo hai hauko vizuri, na wameshauriwa hatua za kuchukua kuwa na mbinu thabiti.

Akizungumzia soko la kilimo cha mboga na matunda alisema bado kunachangamoto soko la ndani na nje kwa wakulima kusafirisha mazao na bidhaa zao.

"Juhudi mbalimbali zimefanyika, tumeshajua mahitaji ya soko kwenye nchi mbalimbali na sampuli ya mazao yameshapelekwa na zimeshaonyesha utayari mkubwa wa kuchukua bidhaa kutoka kwetu," alisema.

Aidha, alisema pia kuna changamoto ya kuwaweka wakulima pamoja, ili kuzalisha bidhaa kwa mujibu wa soko, ikiwamo kiwango na uendelevu wa uzalishaji wa mazao.

Alisema changamoto hiyo wameijadili na kuwekea mikakati kwa wakulima wanaozalisha kwa viwango na uendelevu wa kuzalisha mazao kwa mujibu ya matakwa ya soko.

Naye Ofisa Mradi wa Jumuiya wa Wakulima wa Matunda na Mboga Zanzibar (UWAWIMA), Khamis Issa Muhammed, alisema kuna mabadiliko duniani kwa watu kupenda mazao ya kilimo hai, huku akiwataka wakulima kuacha kutumia mbolea za viwandani.

Alisema mbolea zenye kemikali zinaathiri mazingira afya na mambo mengine, na Zanzibar kwa kiasi kikubwa imeathirika na matumizi ya mbolea za viwandani.

"Tukiangalia hivi sasa Zanzibar tumeathirika asilimia kubwa sana na ukienda Dar es Salaam katika hospitali ya saratani utakuta wagonjwa wanaotoka Zanzibar, wengi ni matumizi ya kemikali," alisema.

Aidha, alisema kilimo hai kina afya nzuri kwa binadamu na kulingana na ardhi ndogo ya kilimo Zanzibar suluhisho ni kilimo hai, ili kutunza mazingira na afya za binadamu.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Idara ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, Haji Sheha, alibainisha changamoto zilizoko kwenye utekelezaji wa mradi huo ni uratibu wa uzalishaji na uendelezaji wa kilimo hicho na wakulima kuzalisha na kusafirisha mwenyewe badala ya kutumia umoja ambao unawapa nguvu.

Aliyataja mafanikio kuwa ni pamoja na kuwafikiwa wakulima wengi ambao wameelimishwa na kupewa nyenzo za kurahisisha kazi yao.

Mradi huo unatekelezwa na taasisi tatu zisizo za kiserikali ambazo ni People's Development Forums (PDF), Community Forests Pemba (CFP) na Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania, Zanzibar (TAMWA-Zanzibar) kupitia mpango wa AGRI-CONNECT kwa ufadhili wa Umoja wa Ulaya (EU).

# Watumishi wafurahia nyongeza mpya ya mshahara

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

CHAMA cha Walimu Zanzibar (ZATU), kimeipongeza Serikali ya Zanzibar kwa kuongeza mishahara watumishi wa umma ambayo imesaidia katika kuinua hali zao kimaisha.

Akizungumza na waandishi wa habari mjini hapa, Katibu wa ZATU, Haji Juma Omar, alisema pamoja na nyongeza hiyo, alikumbusha madai ya stahiki za posho na nauli za walimu ambayo yamecheleweа kwa muda mrefu.

Kwa mujibu wa Omari, walimu wa shule za sekondari wanadai fedha za nauli tangu Agosti 2021 hadi sasa na shule za msingi tangu mwaka 2019.

Alisema Chama cha Walimu kinaridhika na nia njema ya Rais Dk. Hussein Mwinyi, kuboresha maslahi ya wafanyakazi na kutatua changamoto zinazowakabili visiwani humo, ili kuongeza morali ya kazi.

"Wako walimu ambao wameingiziwa taarifa ya kiwango cha elimu ambacho kiko chini kuliko elimu waliyonayo na pia wapo ambao mwaka wao wa ajira haupo sahihi," alifafanua.

Alisema ili kutatua tatizo hilo wamekubaliana na Wizara ya Katiba, Sheria na Utumishi kuwa wafanyakazi wote wajaze fomu maalum, iliyoandaliwa yenye taarifa zinazohitajika katika utoaji wa mishahara.

Aliwataka walimu kujaza fomu hizo kwa usahihi, ili kuondoa dosari iliyojitokeza isijirejee.

"Tunaiomba serikali kulifanyia kazi kwa haraka tatizo hili la nauli za walimu wanazodai kwa sababu muda ni mrefu sana," alisema.

Pia aliomba serikali kuwaongezea posho walimu wakuu ambao kwa sasa hailingani na nafasi wanayoitumikia.

Aidha, alisema kiwango cha posho wanaolipwa walimu wakuu hakizidi Sh. 50,000 wakati walimu wakuu Tanzania Bara wanalipwa wastani wa Sh. 300,000.

# Wanufaika TASAF wachimba bwawa kunywesha mifugo

**Na Shaban Njia,** MBOGWE

BAADHI ya wafugaji wa Kijiji cha Ngemo, Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe mkoani Geita, ambao ni wanufaika wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), wamechimba bwawa la kunyweshea mifugo yao ili kuondokana na kero ya kukamatwa mifugo na askari wa pori la Hifadhi ya Lwamgasa.

Bwawa hilo pia litatumika kwa ajili ya kilimo cha bustani za mboga, matunda na kuwakwamua wananchi hao dhidi ya umaskini.

Mkazi wa kijiji hicho, Masumbuko Amosi, aliyabainisha hayo wakati alipotembelewa na maofisa wa TASAF wilayani humo kuangalia shughuli mbalimbali zinazofanywa na wanufaika wa mpango wa kunusuru kaya maskini unaoratibiwa na TASAF.

Alisema kabla ya kuwapo kwa bwawa hilo walikuwa wakipeleka mifugo yao katika pori la Hifadhi la Lwamgasa kunywesha mifugo yao na kusababisha kuwakamata.

"Niwashukuru wanufaika wa TASAF kijijini kwetu kwa kuona umuhimu wa kuchimba bwawa hili la maji ambalo tunalitumia kwa matumizi ya kilimo na kunyweshea mifugo yetu, nasi tutalitunza ili lisije likajaa matope na kusababisha maji yakapungua na mifugo yetu ikahangaika tena," aliongeza.

Mkazi wa kijiji hicho, Bujiku Malulu, alisema baada ya kuchimbwa kwa bwawa hilo alilazimika kununua hekari 1.5 na kuanza shughuli ya kilimo cha matikiti maji, nyanya, vitunguu, mahindi na maharagwe.

Msimamizi wa bwawa hilo, Fatuma Selemani, mnufaika wa TASAF alisema, walilichimba mwaka jana ili kuanzisha shughuli za kilimo cha umwagiliaji na kuwasaidia wafugaji kunywesha mifugo yao.

Aliwaomba wafugaji kuchimba na kuondoa matope ndani ya bwawa hilo ili kuongeza kina.

Kwa upande wake, Mtendaji wa Kata ya Ngemo, Halmashauri ya Mbogwe, Bahati Laurent, alisema kwa sasa malalamiko ya wafugaji kukamatiwa mifugo yao ndani ya Hifadhi ya Lwamgasa yamepungua baada ya kupata eneo la kunyweshea mifugo yao bure bila malipo.

Alisema baadhi ya wafugaji walilazimika kuchimba visima vifupi jirani na makazi yao na walikuwa wakichangia maji hayo na wanyama wanaowafuga, lakini baada ya walengwa wa TASAF kuchimba bwawa hilo limekuwa msaada kwa kuwa wengi wanatumia pia kwa matumizi ya nyumbani.



Mkuu wa Wilaya ya Magu, Salum Kali (kulia), akikabidhi funguo kwa mshindi wa Bajaj wa promosheni ya Vodacom M-Pesa Imeitika kutoka Mwanza, Hiana Ibrahim, wakati wa hafla ya wiki ya pili iliyofanyika viwanja vya stendi ya Posta jijini humo. Katikati ni Mkuu wa Mauzo Vodacom Kanda ya Ziwa, Ayubu Kalufya. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wafugaji washauriwa kutumia chanjo zaidi

**Na Julieth Mkireri,** CHALINZE

MENEJA Masoko Kiwanda cha kuzalisha chanjo cha Hester kilichoko Kibaha, mkoani Pwani amesema ni vyema wafugaji wakajikita zaidi kwenye chanjo za mifugo badala ya dawa za kutibia.

Dk. Kilmory Ryoba, aliyasema hayo juzi mjini hapo alipokuwa akizungumzia umuhimu wa kutumia chanjo kwa mifugo badala ya dawa.

Alisema wananchi hususani wafugaji wametakiwa waanze kutumia njia ya kuwapa chanjo mifugo yao badala ya dawa ambazo sio nzuri kwa afya za binadamu.

Alisema matumizi ya dawa yaliyokithiri kwenye mifugo yanaweza kuwa chanzo cha kansa kutokana na mabaki ya dawa kwa wanyama.

Kadhalika, Dk. Ryoba alisema, Tanzania ina wanyama wengi, lakini hawawezi kutengeneza soko kutokana na idadi kubwa ya mifugo inayoingia sokoni ikiwa bado na mabaki dawa kwenye nyama.

"Waanze kuegemea kwenye matumizi ya kinga ambayo ni chanjo badala ya kusubiri watumie dawa kutibu kama ilivyo sasa ambavyo yanachangia kukosekana kwa soko kwani nyama na mayai zinaingia sokoni zikiwa na dawa," alisema.

Alisema wanaendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu matumizi ya chanjo badala ya dawa ili wanyama wanaopelekwa sokoni wafikie asilimia 80 hadi 90 wakiwa hawana mabaki ya dawa badala ya kiasi kidogo kilichopo sasa.

Alisema hasara nyingi kwa wafugaji zinatoka kwenye magonjwa hivyo ni vema wakatumia chanjo kuondokana na gharama wanazotumia kutibia mifugo yao.

**Waanze kuegemea kwenye matumizi ya kinga ambayo ni chanjo badala ya kusubiri watumie dawa kutibu kama ilivyo sasa ambavyo yanachangia kukosekana kwa soko kwani nyama na mayai zinaingia sokoni zikiwa na dawa.**

# DC atoa siku 30 wavamizi ardhi kuomba kibali

**Na Thobias Mwanakatwe,** IKUNGI

MKUU wa Wilaya ya Ikungi mkoani Singida, Jerry Muro, ametoa siku 30 kwa wananchi waliovamia maeneo ya ardhi na kuyatumia bila kuomba katika kijiji chochote, waombe kuyatumia kwa uongozi wa kijiji cha Ulyampiti kata ya Unyahati au waondoke.

Alitoa agizo hilo juzi wakati akizungumza na wananchi wa vijiji vya Ulyampiti na Mwau, vilivyoko kata za Unyahaati na Mang'onyi pamoja na wananchi waliowekeza kwenye shamba la pamoja la kilimo cha korosho lenye hekari elfu tatu.

Muro alisema wananchi waliovamia wawapishe waliolipia maeneo hayo kwa ajili ya kilimo cha korosho na tayari Halmashauri ya Kijiji cha Ulyampiti wameshakusanya zaidi ya Sh. milioni 51 kutoka kwa wananchi wanaotaka kuwekeza kwenye kilimo hicho.

Mkuu huyo wa wilaya alilazimika kutoa ufafanuzi wa mgogoro wa mpaka wa vijiji hivyo na kusema kwa mujibu wa vipimo vya kitaalamu eneo lenye hekari 3,000 liko kijiji cha Ulyampiti.

Alisema wananchi waliomba kwa maandishi kupitia kijiji cha Mwau kukaa kwenye maeneo hayo wasiondolewe na uongozi wa kijiji cha Ulyampiti kwa kuwa changamoto imesababishwa na viongozi wa Kijiji cha Mwau kutokufuata utaratibu na wananchi waliopewa kwa maandishi maeneo hayo wabaki walipo na wasisumbuliwe.

Muro alisema kwa mwananchi yeyote anayetaka kuishi kwenye eneo hilo la mradi lazima aombe kwa maandishi na awe tayari kulipia gharama za kupewa ardhi na uongozi wa kijiji cha Ulyampiti.

Aliwaonya baadhi ya wananchi na viongozi kutoka kijiji cha Mwau kuacha tabia ya kuvamia mashamba hayo na kuchoma moto mikorosho iliyopandwa na wananchi waliowekeza katika eneo hilo.

HABARI KIMATAIFA

## Mama, watoto wafungiwa ndani miaka 17

**RE DE JANEIRO,** Brazil

MWANAMKE mmoja wa Brazil amesimulia jinsi alivyofungiwa ndani na kuteswa pamoja na watoto wake wawili kwa miaka 17.

Tukio hilo la kusikitisha limefanywa na mume wake kwa kipindi chote bila kujulikana na mtu yeyote.

Hata hivyo, mwanamke huyo aliokolewa Alhamisi iliyopita kutoka ndani ya nyumba hiyo iliyoko katika kitongoji cha Guaratiba, magharibi mwa Rio de Janeiro nchini Brazil.

Mume wake ambaye anatuhumiwa kuwafungia ndani familia yake amekamatwa. Katika taarifa iliyonukuliwa na tovuti ya habari ya Brazil G1, mwanamke huyo alidai kuwa mumewe alisema hawataweza kutoka ndani ya nyumba hiyo, hadi hapo atakapofariki dunia.

Kulingana na polisi, mwanamume huyo aliyetajwa kwa jina la Luiz Antonio Santos Silva na mkewe walikuwa wameoana miaka 23 iliyopita.

Baada ya kuokolewa, inasemekana mama huyo aliiambia mamlaka kwamba kuna wakati walikaa bila chakula kwa kwa siku tatu, na mara nyingi walinyanyaswa kimwili na kisaikolojia.

Nyumba walimofungwa pia ilikuwa mbovu, yenye mwanga mdogo na mazingira ya ndani ni machafu, picha zilizotolewa na polisi zinaonyesha.

Polisi walisema waliwakuta watoto hao wawili wakiwa katika hali mbaya ya kukomaa, walifungwa kamba na wakiwa na njaa.

Watoto hao wana umri wa miaka 19 na 22, ripoti ya vyombo vya habari ilieleza. **BBC**

## Hasira zaibuka mauaji ya mtu mweusi Italia

**MILAN,** Italia

KIFO cha mhamiaji mmoja Mwafrika aliyeshambuliwa mchana nchini Italia kimeibua hasira duniani kote.

Shambulio dhidi ya mfanyabiashara huyo raia wa Nigeria, lililotekelezwa mtaani na mwanamume wa kizungu katika kituo cha mji wa Civitanova Marche, lilinaswa katika video na watu waliokuwa karibu na tukio hilo.

Video hiyo, iliyochukuliwa na watazamaji ambao hawakutoa msaada wowote wa kumwokoa, inaonyesha Mwafrika huyo akiwa ameshikiliwa na raia mmoja mzungu.

Tayari Muitaliano mwenye umri wa miaka 32 amekamatwa kwa tuhuma za mauaji na wizi.

Video ya shambulio hilo ambayo imesambaaa kwenye tovuti za habari za Italia na mitandao ya kijamii, imeshtua jamii, huku wengi wakionyesha 'kutojali kile kilichotokea.

Mtu aliyeuawa ametajwa kuwa Alika Ogorchukwu, ameoa na ana watoto wawili. **BBC**

KINACHOJIRI UKRAINE



Mwanajeshi wa Ukraine akijibu mashambulizi kwa kufyatua kombora katika mtambo uliotolewa na Marekani juzi. **PICHA: REUTERS**

# Rais Zelenskiy aamuru raia kuondoka Donesk

**Kyiv,** UKRAINE

RAIS wa Ukraine, Volodymyr Zelenskiy, amewaamuru watu kuondoka mara moja katika eneo la mashariki la Donetsk.

Kauli hiyo ameitoa wakati jeshi la nchi hiyo likidai kuua askari wengi wa Russia katika mji wa Kherson.

Rais Zelenskiy aliamuru kuhamishwa kwa watu kutoka eneo la Donetsk ambalo limeshuhudia mapigano makali kati ya vikosi vya Russia na Ukraine.

"Tayari kuna uamuzi wa serikali kuhusu uhamishaji wa lazima kutoka mkoa wa Donetsk," Zelenskiy alisema katika hotuba yake ya kila siku ya video ya jana

"Tafadhali, fuateni utaratibu wa uhamishaji. Katika awamu hii ya vita, ugaidi ni silaha kuu ya Russia." Alisisitiza.

Alisema mamia kwa maelfu ya watu bado wanaishi katika maeneo ya Donbas ambako mapigano yalikuwa makali.

"Ikiwa utapata fursa, tafadhali zungumza na wale ambao bado wamesalia katika maeneo ya mapigano huko Donbas. Tafadhali washawishi kwamba ni muhimu kuondoka, haswa ikiwa ni familia zenye watoto. Ukipata fursa ya kusaidia watu waliohamishwa, fanya hivyo," aliongeza katika hotuba yake.

Zelensky aliahidi msaada wa vifaa na pesa taslimu kusaidia raia wanaohamishwa.

Katika matukio tofauti, vyombo vya habari vya Ukraine vilimnukuu Naibu Waziri Mkuu Iryna Vereshchuk, akisema uhamishaji unahitajika kufanyika kabla ya msimu wa baridi kuanza kwa sababu usambazaji wa gesi asilia katika eneo hilo uliharibiwa.

Juzi jeshi la Ukraine lilisema zaidi ya wanajeshi 100 wa Russia waliuawa na vifaru saba kuharibiwa katika mapigano yaliyotokea kusini Ijumaa.

Eneo hilo ni pamoja na Kherson ambako ndiyo shabaha ya kujibu mashambulizi ya Ukraine.

Mji huo ni kiungo muhimu katika njia za usambazaji wa vifaa kwa vikosi vya Russia.

Usafiri wa reli hadi Kherson kuvuka Mto Dnipro ulikuwa umekatwa, ilisema kamandi ya kusini ya jeshi na kuweka uwezekano zaidi wa kuvitenga vikosi vya Russia vilivyoko magharibi mwa mto na rasi inayokaliwa ya Crimea na mashariki.

Kusini mwa mji wa Bakhmut, ambao Russia imeutaja kama shabaha kuu huko Donetsk, jeshi la Ukraine lilisema kuwa vikosi vya Russia vimefanikiwa kwa kiasi kudhibiti eneo la makazi la Semyhirya kwa kulivamia kutoka pande tatu.

"Wamejiimarisha nje kidogo ya makazi," ripoti ya jana jioni ya jeshi ilisema, ikimaanisha vikosi vya Russia.

### UK: RUSSIA YADUMISHA KASI YA UVAMIZI

Maofisa wa ulinzi na ujasusi wa Uingereza, ambao wamekuwa mmoja wa washirika wakubwa wa Ukraine tangu Russia ilipoivamia Februari 24, walivionyesha vikosi vya Russia kama vinavyohangaika kuongeza kasi.

Ukraine imetumia mifumo ya makombora ya masafa marefu inayotolewa na nchi za Magharibi

kuharibu vibaya madaraja matatu katika Mto Dnipro katika wiki za hivi karibuni, na kuukatia mawasiliano mji wa Kherson na katika tathmini ya maofisa hao kuwa kunatoa nafasi katika kikosi cha 49 cha jeshi la Russia, kuwa katika hatari kwenye ukingo wa magharibi wa mto huo.

Gavana wa mkoa wa Kherson, anayeegemea Ukraine, Dmytro Butriy, alisema mapigano yanaendelea katika maeneo mengi ya eneo hilo, na kwamba wilaya ya Berislav, kaskazini magharibi mwa kiwanda cha kuzalisha umeme cha Kakhovka, kuliathirika sana.

"Katika baadhi ya vijiji, hakuna hata nyumba moja iliyoachwa, miundombinu yote imeharibiwa, watu wanaishi kwenye mahandaki," aliandika kwenye Telegram.

Kaskazini mwa Lysychansk, ambayo vikosi vya Moscow viliiteka mapema Julai baada ya mapigano ya wiki kadhaa, wapiganaji wa Ukraine waliharibu boksi la makutano ya reli karibu na mji unaodhibitiwa na Russia.

Maofisa wa utawala walioteuliwa na Russia, kuendesha mkoa wa Kherson, mapema wiki hii walipinga tathmini za Magharibi na Ukraine kuhusu hali hiyo.

### VIFO VYA GEREZANI

Ukraine na Russia zimetuhumiana kuhusu shambulizi la kombora au mlipuko Ijumaa ambao uliua wafungwa zaidi ya 40 katika mji wa mapambano wa Olenivka, ambao unashikiliwa na waasi wanaoungwa mkono na Russia.

Wizara ya ulinzi ya Russia, ilichapisha orodha ya wafungwa 50 wa kivita wa Ukraine waliouawa na 73 waliojeruhiwa katika kile ilichosema ni shambulio la kijeshi la Ukraine kwa kutumia mfumo wa roketi wa kisasa uliotengenezwa na Marekani (HIMARS).

Msemaji wa wizara hiyo, Luteni Jenerali Igor Konashenkov, alisema wajibu wote wa kisiasa, jinai na maadili unabaki kwa Zelenskiy, serikali yake ya uhalifu na Marekani inayowaunga mkono.

Vikosi vya jeshi la Ukraine vilikanusha kuhusika, vikisema kwamba mizinga ya Russia ililenga jela hiyo ili kuficha unyanyasaji wa wale wanaoshikiliwa humo.

Waziri wa Mambo ya Nje, Dmytro Kuleba, alisema Russia ilifanya uhalifu wa kivita na kutoa wito wa kulaaniwa kimataifa. **DW**

## HABARI MICHEZO

# WAZIRI MKUU AIPONGEZA NBC MSAADA SARATANI YA KIZAZI

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameipongeza Benki ya NBC kwa kuandaa Marathoni ya kuchangisha fedha, "NBC Dodoma Marathoni," kusaidia mapambano dhidi ya saratani ya mlango wa kizazi nchini Tanzania.

**Akizungumza katika mbio za marathoni mjini Dodoma jana, Majaliwa alisema kuwa serikali inathamini jitihada za sekta binafsi za kuungana mkono katika kutafuta ufumbuzi wa changamoto zinazoikabili jamii.**

"Serikali inatambua kazi nzuri ya mchango wa kijamii uliofanywa na Benki ya NBC kwa miaka mingi. Tunashukuru kwa ubunifu wa kushirikiana na Taasisi ya Saratani ya Ocean Road na Chama cha Riadha Tanzania kuendeleza mbio hizi za marathoni zinazolenga kukusanya fedha za kusaidia mapambano dhidi ya saratani ya mlango wa kizazi nchini Tanzania," alisema.


Alisema saratani ya shingo ya kizazi, ingawa inaongoza kwa kupoteza maisha ya wanawake nchini Tanzania, inaweza kuepukika na kutibika iwapo itagundulika mapema.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Theobald Sabi alisema benki hiyo inafuraha kuandaa kipindi kingine cha mbio za NBC Bank Dodoma Marathon baada ya mafanikio mawili hapo jana.

"Baada ya matoleo mawili yenye mafanikio ya mbio za Marathon hapa Dodoma, tunayo furaha kuandaa toleo la tatu. Pesa zote zilizopatikana, karibu Sh. milioni 200, zitaelekezwa katika Taasisi ya Saratani ya Ocean Road kusaidia mapambano ya wanawake dhidi ya saratani ya mlango wa kizazi," alisema.

"Ninayofuraha kutangaza kwamba katika kipindi cha miaka miwili iliyopita, mbio za Marathoni zilikusanya zaidi ya Sh. milioni 300, ambazo zilisaidia kupima wanawake zaidi ya wanawake 9,000, 550 kati yao waligundulika kuwa na saratani na kwa sasa wanaendelea na matibabu. Nashukuru kwa uungwaji mkono wote kutoka pembe zote za bara hili, huku watu wakijumuika nasi katika kazi hii adhimu," alisema.

Alisema Benki ya NBC ina bahati ya kuweza kukusanya fedha ili kuokoa maisha na kuleta matumaini kwa familia.




Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Theobald Sabi, akimkambidhi Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa mfano wa hundi ya Sh. milioni 200 zilizopatikana katika mbio za NBC Bank Dodoma Marathon ambazo lengo kuu ni za kusaidia mapambano dhidi ya saratani ya mlango wa kizazi nchini Tanzania kupitia Taasisi ya Saratani ya Ocean Road. Mbio hizo zilifanyika katika Jiji la Dodoma na kuhitimishwa katika Uwanja wa Jamhuri jana Jumapili. **NA MPIGAPICHA WETU**

# *Kidunda amdunda Katompa*

**Na Saada Akida,** SONGEA

NDEREMO na furaha zilifurika katika ardhi ya mashujaa ya Uwanja wa Majimaji, Songea baada ya bondia wa ngumi za kulipwa nchini, Seleman Kidunda kumchapa mpinzani wake, Tshimanga Katompa raia wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Pambano hilo lilikuwa la raundi 10 la uzito wa Super Middle Weight (KG76) kuwania ubingwa wa WBF Intercontinental huku bondia mwenye mkwara, Karim Mandonga akichezea kichapo kwa TKO kutoka kwa Shabani Kaoneka.

Katika pambano hilo la Pay Back Night ambalo limepigwa kwenye Uwanja wa Majimaji ulioko mjini hapo, Kidunda amefanikiwa kumchapa bondia huyo ambaye mwaka jana alitoka naye sare ya kiufundi.

Kidunda ameshinda pambano hilo kutokana na kuongoza kwa raundi zote huku akimpeleka chini mpinzani wake katika raundi ya tatu, lakini aliweza kuinuka na kuendelea baada ya kuhesabiwa.

Kufuatia ushindi huo, Kidunda amewashukuru Watanzania huku akiutoa ushindi huo kwa mashabiki wote wa mchezo huo kutokana na sapoti kubwa walioweza kumpa wakati wote.

Lakini kwa upande wa Katompa amesikitishwa na kipigo hicho huku akidai kuwa alipuliziwa dawa kwenye chumba chake katika hoteli aliofikia hali iliyopelekea kupoteza pambano hilo.

Wengine walioshinda katika mapambano ya utangulizi ni Shaban Kaoneka aliyemchapa Karim Mandonga kwa TKO ya raundi ya nne, wakati Ismail Galiano akimpiga KO, Buda Chikoko kutoka Malawi na George Bonabucha akimtandika kwa TKO, Yusuph Alli.



## Tshishimbi, Tigere watua rasmi Ihefu

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Timu ya Ihefu FC, umekamilisha dili la wachezaji wawili wa kimataifa, Never Tigere na Papy Tshishimbi kwa mkataba wa mwaka mmoja kuitumikia timu hiyo.

Ihefu inayonolewa na Kocha mzawa Zuberi Katwila imerejea kwa mara nyingine kwenye Ligi Kuu Tanzania baada ya kushuka kwa msimu uliopita.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Ihefu, Zagalo Chalamila, alisema nyota hao wawili wamewasili nchini jana (Jumapili) na kwenda moja kwa moja Mbeya kuungana na wachezaji wenzao walikuwapo kambini.

Alisema wamesajili kwa kuzingatia mahitaji ya benchi la ufundi, lakini mapungufu ya kikosi chao kwa kusajili wachezaji bora na wenye ubora wa kupambania timu.

"Msimu huu Ihefu tumejipanga vizuri kuanzia usajili na hata maandalizi yetu kambini yako vizuri kwa sasa timu iko Mbeya kwa ajili ya kujiimarisha na msimu mpya," alisema Chalamila.

Ihefu imekamilisha usajili wa Ramadhani Ally (KMC), Said Juma (Polisi Tanzania), Lenny Kissu (Biashara United), Juma Nyosso (Geita Gold), Peter Mwalyanzi (Kagera Sugar) na Jaffray Kibaya (Mtibwa Sugar) na Nicolaus Wadada (Azam FC).

## Azam FC yanoa makali mastraika wake

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Azam FC inayoendelea na mazoezi yake nchini Misri, inatilia mkazo zaidi kuwanoa mastraika wake ili waweze kufanya vema kwenye msimu ujao wa mashindano ya ndani na nje ya nchi.

Kocha wa mastraika wa timu hiyo, Kalimangonga Ongala amesema amekuwa wakiwanoa mastraika wote wa kizawa na wa nje ya nchi na alichogundua ni kwamba wana vipaji, isipokuwa wanatakiwa wafanye zaidi mazoezi ya kufunga ili wazoee.

"Nafanya mazoezi na mastraika, sina tatizo na vipaji vyao, ila ni kujizoesha kufunga. Ukijizoesha kufunga kwenye mazoezi utafunga kwenye mechi, ukikosa kufunga kwenye mazoezi, kwenye mechi nako utashindwa kufunga. Kwa hiyo tunachofanya sasa ni kuwaboresha mastraika wetu ili ligi ikianza iwe kwao ni kawaida tu kutupia," alisema Kally, straika wa zamani wa Abajalo, Yanga na Kajumulo.

Naye Ofisa Habari wa klabu hiyo, Thabit Zacharia, amesema Kocha Mkuu, Abdihamid Moalin amekuwa na kazi ya kutengeneza muunganiko kati ya wachezaji wapya na wale wa zamani.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### WERNER ATAJWA NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle United iko kwenye mazungumzo na Chelsea kuhusu mkataba wa mkopo wa mshambuliaji wa Ujerumani Timo Werner, 26, ambaye amekuwa akihusishwa na klabu ya zamani ya RB Leipzig. ***(Sunday Mirror)***

### CUCURELLA BASI TENA

KLABU ya Brighton haitafanya mazungumzo tena na Manchester City kuhusu kumuuza beki wa kushoto wa Hispania, Marc Cucurella, 24. ***(Athletic)***

### MADDISON BEI GHALI

KLABU ya Leicester City inataka zaidi ya pauni milioni 50 ili kumuuza mchezaji wa England, James Maddison, 25, kwa Newcastle United, ambao dau la pauni milioni 40 kwa mchezaji huyo limekataliwa. ***(Times)***

### HOWE HAJAZUNGUMZA

KOCHA wa Newcastle United, Eddie Howe hakuzungumzia lolote kuhusu uhamisho wa James Maddison, lakini alisema anatumaini kuongeza kikosi chake kabla ya kuanza msimu dhidi ya Nottingham Forest, Agosti 6. ***(Northern Echo)***

### CORNET AWANIWA

KLABU ya Newcastle imefanya mawasiliano na Burnley kuhusu Maxwel Cornet, lakini bado hawajatoa ofa kwa winga huyo wa Ivory Coast mwenye umri wa miaka 25. ***(90 Min)***

### ARRIZABALAGA KWA MKOPO

CHELSEA wanakaribia kufikia makubaliano ambayo yatamfanya mlinda mlango wa Hispania, Kepa Arrizabalaga ajiunge na Napoli ya Italia kwa mkopo msimu huu.***(Mail)***

### AZPILICUETA, ALONSO NA BARCA

BARCELONA inataka kuwasajili, Cesar Azpilicueta, 32 na Marcos Alonso mwenye miaka 31 kutoka Chelsea wiki ijayo. ***(Sport)***

### ARTETA KUSAJILI ZAIDI

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta amesema anataka kikosi chake kuongezwa zaidi msimu huu, huku washikabunduki hao wakiwa na nia ya kumnunua kiungo wa kati wa Leicester City na Ubelgiji, Youri Tielemans, 25. ***(90 min)***

### KETELAERE KUTUA MILAN

AC Milan imekubali kumsajili kiungo wa kati wa Ubelgiji, Charles de Ketelaere, 21, kutoka Club Bruges kwa pauni milioni 26.9. Mchezaji huyo pia amekuwa akihusishwa na Leeds United. ***(Calciomercato)***

### MUKIELE ATUA PSG

KLABU ya Paris St-Germain imemsajili beki Nordi Mukiele, 24, kutoka RB Leipzig kwa mkataba wa miaka mitano. Beki wa kulia wa Ufaransa amesema alikataa kwenda Chelsea. ***(L'Equipe, via Metro)***

### CASADEI ATAKIWA

CHELSEA imetoa ofa ya pauni milioni 6.7 kwa kiungo wa kati wa Italia, Cesare Casadei mwenye umri wa miaka 19. ***(Gazzetta)***

## DONDOO ZA SOKA
## MAGA… A ULAYA



# GUARDIOLA: HAALAND ATAFUNGA SIKU NYINGINE

**● ● ● Ni baada ya kukosa nafasi za wazi wakati City ikilala...**

**LONDON,** England

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, amesisitiza kwamba, mchezaji aliyesajiliwa majira ya joto, Erling Haaland atafunga 'siku nyingine' baada ya mshambuliaji huyo nyota kukosa nafasi nyingi kwenye mchezo dhidi ya Liverpool wa Ngao ya Jamii, Jumamosi.

**Haaland aliwasili City akiwa amefunga mabao 134 katika mechi 137 alizoichezea klabu na nchi tangu kuanza kwa msimu wa 2019/20.**

Lakini raia huyo wa Norway mwenye umri wa miaka 21 alishindwa kufunga katika mashuti yake matatu wakati Liverpool ikiibuka na ushindi wa 3-1.

Akizungumza baada ya mchezo huo, Guardiola alisema Haaland bado anahitaji kuwa fiti baada ya kurejea uwanjani, kwani alikosa sehemu mbili za msimu uliopita akiwa na Borussia Dortmund kwa sababu ya jeraha.

"Alipata nafasi mbili au tatu katika kipindi cha kwanza na moja mwishoni. Daima alikuwa huko. Alipigana sana na kufanya harakati," alisema Guardiola.

"Ni vizuri kwake kuona kwani yupo kwenye nchi mpya na ligi mpya. Alikuwapo. Leo (juzi) hakufunga - siku nyingine atafunga."

City wataanza msimu wa Ligi Kuu ugenini dhidi ya West Ham Jumapili ya Agosti 7.

Kikosi cha Guardiola kitakabiliana na Bournemouth na Nottingham Forest waliopanda daraja kabla ya mwisho wa mwezi na hawatakutana na mojawapo ya timu nne bora za msimu uliopita hadi watakapowakaribisha Tottenham Hotspur katika mechi ya wiki ya saba.

Mechi ya marudiano na Liverpool itafuatia wiki chache baadaye katikati ya Oktoba.

BREAKING NEWS
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,019,3

JACKPOT
MECHI WIKI HII
TAREHE: 06 AGOSTI 2022
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 03/08/22 | 20:00 | Landskrona Bois vs Skovde Aik | 2.28 | 3.47 | 3.01 |
| 02. 03/08/22 | 20:00 | Dalkurd FF vs Norrby IF | 2.96 | 3.57 | 2.26 |
| 03. 03/08/22 | 21:30 | Dunajska Streda vs Steaua Bucuresti | 2.62 | 3.33 | 2.57 |
| 04. 04/08/22 | 03:00 | Juarez FC vs San Luis | 2.52 | 2.92 | 2.97 |
| 05. 04/08/22 | 18:30 | AEK Larnaca vs Partizan | 3.17 | 3.22 | 2.25 |
| 06. 04/08/22 | 19:00 | Stjordals-Blink vs Grorud IL | 2.60 | 3.43 | 2.36 |
| 07. 04/08/22 | 19:00 | Sandnes Ulf vs Sogndal | 2.33 | 3.48 | 2.60 |
| 08. 04/08/22 | 19:30 | Spartak Trnava vs Rakow Czestochowa | 3.02 | 3.33 | 2.28 |
| 09. 04/08/22 | 20:00 | Jonkopings Sodra vs Vasteras SK | 2.40 | 3.57 | 2.76 |
| 10. 04/08/22 | 20:30 | Zorya Lugansk vs Universitatea Craiova | 2.62 | 3.18 | 2.67 |
| 11. 04/08/22 | 21:00 | Sepsi Osk vs Djurgardens IF | 2.58 | 3.24 | 2.68 |
| 12. 04/08/22 | 21:30 | Brondby vs FC Basel | 2.56 | 3.37 | 2.61 |
| 13. 04/08/22 | 22:00 | Hajduk Split vs Vitoria Guimaraes | 2.57 | 3.33 | 2.62 |

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
BREAKING
airtel money
EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249
18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# MANE ATAKA MATAJI ZAIDI BAYERN



**MUNICH,** Ujerumani

SADIO Mane analenga kutwaa mataji zaidi baada ya kufunga bao lake la kwanza la ushindani akiwa na Bayern Munich katika ushindi wa taji la Super Cup dhidi ya RB Leipzig, Jumamosi.

Bayern walishinda 5-3 kwenye mchezo huo wa kufungua pazia la ligi, huku Mane akichukua muda mfupi sana kufungua akaunti yake ya mabao kwa mabingwa hao wa Bundesliga baada ya uhamisho wake wa pauni milioni 35 kutoka Liverpool mapema msimu huu wa joto.

Baada ya Jamal Musiala kufunga bao la kwanza kwenye Uwanja wa Red Bull Arena, Mane alipewa nafasi ambayo hangeweza kuikosa na akafunga.

Serge Gnabry alitoka na mpira kushoto na kumtengenezea pande zuri mchezaji huyo wa zamani wa Liverpool, ambaye alikuwa katikati ya walinzi wa Leipzig na akafanikiwa kufunga.

Akizungumza baada ya mechi hiyo, Mane alifichua kuwa tayari alikuwa akiishi na 'ndoto' hiyo mjini Munich na analenga kupata mataji zaidi.

"Nina furaha sana kufunga bao langu la kwanza kwa Bayern," alisema. "Hii ni ndoto yangu. Natarajia mataji zaidi.



## McCarthy ateuliwa kocha Man U

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester United imethibitisha uteuzi wa Benni McCarthy kama kocha wa kikosi cha kwanza, akijiunga na Erik ten Hag hapo Old Trafford.

Mshambuliaji huyo wa zamani wa Porto, Ajax, Blackburn Rovers na West Ham alikuwa shabiki wa Man United tangu utotoni na amejiunga na benchi la ufundi la kikosi hicho ambapo atakuwa na kazi ya kuwanoa washambuliaji.

McCarthy awali alikuwa kocha mkuu wa klabu ya AmaZulu ya Afrika Kusini, lakini alijiuzulu Machi mwaka huu, baada ya kukiongoza kikosi hicho kushika nafasi ya pili kwenye Ligi Kuu.


Hilo lilimpelekea kutajwa kuwa Kocha Bora wa Ligi Kuu ya Afrika Kusini kwa msimu wa 2020-21.

"Ninaiunga mkono Man United na siku zote nilitaka kuichezea. Nilipenda wachezaji kama Mark Hughes, Andy Cole na Ryan Giggs," alisema McCarthy akinukuliwa na tovuti rasmi ya klabu hiyo.

Uteuzi wa McCarthy mwenye umri wa miaka 44 unakamilisha kikosi cha Ten Hag kabla ya kampeni yake ya kwanza hapo Old Trafford, akijiunga na wachezaji wengine wa zamani kama Mitchell van der Gaag, Steve McLaren, Eric Ramsay na Darren Fletcher.

301,493/-

# NABI AWACHIMBA MKWARA WACHEZAJI



**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Nesreddine Nabi kama amewachimbia mkwara nyota wake wapya kwa kuwaeleza hakuna staa mkubwa katika kikosi cha timu hiyo na kutaka watengeneze timu.

**Yanga inaendelea na maandalizi katika kambi yao ya Avic Town iliyoko Kigamboni kwa ajili ya msimu mpya wa kimashindano huku wakianzia kufungua Ligi Kuu Tanzania Bara kwa mchezo dhidi ya Simba.**

Kwa mujibu wa Nabi alisema wachezaji wa msimu uliopita wanaifahamu falsafa yake na kuhakikisha nyota wapya nao wanatambua hilo kwa kila mmoja yuko sawa na mwenzake.

Alisema anachotambua mchezaji yeyote aliye katika kikosi cha timu hiyo ni kuijenga Yanga kuwa imara na kupata matokeo mazuri ni kila mmoja kujituma na kujitoa kwa ajili ya kupambania malengo.

"Nasimama katika nidhamu hakuna mkubwa ndani ya Yanga, tuko hapa kwa ajili ya kutengeneza timu kuwa moja na kushirikiana ili kufikia malengo ikiwamo kutetea mataji yetu yote matatu," alisema Nabi.

Alisema ndani ya timu yake hakuna mchezaji aliyekuwa juu akiamini wote wamesajiliwa kwa ajili ya kufikisha malengo yao ya kutwaa mataji yao kwa mara ya pili mfululizo.

Nabi alisema endapo wachezaji wakijiona wao wakubwa ndani ya klabu hiyo ana imani hatawafika malengo yao kwa sababu kufikia huko lazima nidhamu na ushirikiano kwa kila mchezaji.



Mkuu wa Wilaya ya Bunda, Joshua Nassari (wa nne kulia), akiwa pamoja viongozi na wadau waliosaidia mbio za Serengeti Migration Marathon. Kulia waliokaa ni Katibu wa Riadha Mkoa wa Mara, Vedastus Makaranga, Meneja Mauzo wa Kampuni ya Serengeti Breweries Mara na Simiyu, Jay Jay Mwarabu Gombanilla, Mwenyekiti wa riadha Mara, Deogratias Misana, na (kushoto) ni Geofrey Werema mwandaaji wa mbio, Said Babu Mwenyekiti wa Rufani Riadha Wilaya na Katibu Tawala wa Serengeti, Cosmas Qamara. Waliosimama ni baadhi ya waandaaji wa mbio hizo zilizofanyika viwanja vya Sokoine Mugumu Julai 30. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# *UWERFA kufanya marekebisho*

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

CHAMA cha Mpira wa Miguu Mkoa wa Mjini Magharibi (UWERFA) kimesema msimu mpya wa ligi kimejipanga kufanya maboresho makubwa katika ligi yake ya Mkoa.

Akizungumza na gazeti hili Katibu Mkuu wa chama hicho, Ahmada Haji Khamis, alisema miongoni mwa maboresho hayo ni kuhakikisha kufanya Ligi ya Mkoa wa Mjini Magharibi kuwa yenye ushindani wa hali ya juu ikilinganishwa na misimu mitatu iliyopita tangu kuundwa kwa ligi hiyo ya mkoa.

Alisema miongoni mwa mambo yatakayoboreshwa ni kutafuta wadhamini wa ligi hiyo, lakini kutoa elimu kwa viongozi wa klabu na namna bora ya uendeshaji.

"Tunaendelea na kutafuta wadhamini wa ligi ya mkoa wa Mjini Magharibi, ambapo tumefikia hatua nzuri na wafanyabiashara ambao tumewafuata na kuona kiasi gani watafaidika endapo watatudhamini," alisema.

Aidha alisema kupatikana kwa wadhamini wa ligi kutaleta hamasa zaidi kwa klabu kucheza soka safi huku wakijua bingwa wa ligi hiyo nini atapata mwisho wa msimu.


## SUPA JACKPOT
## MECHI WIKI HII
### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 06/08/22 | 17:00 | Leeds vs Wolverhampton | 2.29 | 3.29 | 3.09 |
| 02. 06/08/22 | 17:00 | Bristol City vs Sunderland | 2.21 | 3.24 | 3.29 |
| 03. 06/08/22 | 17:00 | QPR vs Middlesbrough | 2.47 | 3.24 | 2.84 |
| 04. 06/08/22 | 17:00 | Reading vs Cardiff | 2.44 | 3.18 | 2.94 |
| 05. 06/08/22 | 17:00 | Swansea vs Blackburn | 2.36 | 3.19 | 3.04 |
| 06. 06/08/22 | 17:00 | Burton vs Bristol Rovers | 2.39 | 3.33 | 2.88 |
| 07. 06/08/22 | 17:00 | Charlton vs Derby | 2.79 | 3.19 | 2.54 |
| 08. 06/08/22 | 17:00 | Exeter vs Port Vale | 2.53 | 3.17 | 2.82 |
| 09. 06/08/22 | 17:00 | Fleetwood Town vs Plymouth | 2.84 | 3.24 | 2.48 |
| 10. 06/08/22 | 17:00 | MK Dons vs Sheffield Wed | 2.61 | 3.21 | 2.71 |
| 11. 06/08/22 | 17:00 | Shrewsbury vs Accrington | 2.53 | 3.23 | 2.78 |
| 12. 06/08/22 | 17:00 | Barrow vs Bradford City | 2.59 | 3.13 | 2.78 |
| 13. 06/08/22 | 17:00 | Crawley Town vs Leyton Orient | 2.58 | 3.22 | 2.73 |
| 14. 06/08/22 | 17:00 | Hartlepool vs AFC Wimbledon | 2.89 | 3.24 | 2.44 |
| 15. 06/08/22 | 17:00 | Mansfield vs Tranmere | 2.26 | 3.19 | 3.24 |
| 16. 06/08/22 | 18:00 | Strasbourg vs Monaco | 2.73 | 3.23 | 2.53 |
| 17. 06/08/22 | 21:30 | Hansa vs Arminia Bielefeld | 2.64 | 3.34 | 2.59 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMATATU - 01 - AGOSTI 2022

| MUDAVV | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:30 | 2450 | Seoul E Land vs Gimpo Citizen | 1.86 | 3.39 | 3.73 |
| 13:30 | 2728 | Bucheon vs Gyeongnam | 2.50 | 3.09 | 2.65 |
| 15:15 | 1062 | Johor Darul Takzim vs Kuala Lumpur | 1.18 | 6.25 | 10.74 |
| 16:00 | 1218 | Pahang FA vs Kedah | 2.46 | 3.64 | 2.39 |
| 16:00 | 5095 | San Lorenzo de Almagro Res. vs Argentinos Juniors Reserve | 3.35 | 3.25 | 2.03 |
| 16:00 | 5553 | Terengganu vs FC Petaling Jaya City | 1.42 | 4.43 | 5.91 |
| 16:30 | 5340 | Persebaya Surabaya vs Persita Tangerang | 1.56 | 3.70 | 5.33 |
| 17:00 | 4324 | Surkhon Termez vs FC Olimpik | 2.08 | 2.75 | 3.92 |
| 17:00 | 5352 | Valerenga IF 2 vs Brattvag | 2.64 | 3.82 | 2.17 |
| 18:00 | 2279 | FK Auda vs Valmiera Fk/Bjss | 5.10 | 3.92 | 1.54 |
| 18:00 | 2682 | Hifk vs Inter Turku | 4.21 | 3.58 | 1.72 |
| 18:00 | 2782 | Pakhtakor vs Dinamo Samarqand | 1.11 | 7.05 | 18.59 |
| 18:00 | 4429 | Sogdiyona Jizzax vs Bunyodkor | 1.88 | 3.25 | 3.84 |
| 18:30 | 4272 | FK Zeleznicar Pancevo vs FK Zlatibor | 1.66 | 3.40 | 5.60 |
| 19:00 | 2144 | Nieciecza KS vs GKS Tychy | 1.74 | 3.45 | 4.23 |
| 19:00 | 3819 | Drogheda Utd vs UCD Dublin | 1.70 | 3.62 | 4.21 |
| 19:01 | 1384 | Energie Cottbus vs Werder Bremen | 10.20 | 6.32 | 1.24 |
| 19:01 | 4084 | Chemnitz vs Union Berlin | 16.28 | 7.33 | 1.16 |
| 19:01 | 4227 | Ingolstadt vs SV Darmstadt | 3.82 | 3.62 | 1.92 |
| 19:15 | 5459 | KP Polonia Warsaw vs Stomil Olsztyn | 1.81 | 3.54 | 3.78 |
| 19:30 | 1172 | National Bank vs El Gouna | 2.04 | 3.11 | 3.81 |
| 19:30 | 5584 | Ismaily SC vs Misr Lel Makasa | 1.57 | 3.66 | 6.01 |
| 19:45 | 3275 | Umm-Salal SC vs Al Ahli Doha SC | 2.12 | 3.34 | 3.04 |
| 20:00 | 1114 | Angelholms vs Lunds BK | 1.63 | 3.77 | 4.50 |
| 20:00 | 1668 | Korona Kielce vs Slask Wroclaw | 3.14 | 3.24 | 2.12 |
| 20:00 | 1756 | Vindbjart vs Express IL | 1.44 | 4.82 | 5.11 |
| 20:00 | 2122 | Rubin Kazan vs Ufa | 2.26 | 3.25 | 2.86 |
| 20:00 | 2796 | Nordsjalland vs Lyngby | 1.64 | 3.81 | 4.91 |
| 20:00 | 3209 | Hassleholms IF vs Nosaby IF | 1.54 | 4.12 | 4.81 |
| 20:00 | 3567 | IFK Goteborg vs Norrkoping | 2.46 | 3.30 | 2.56 |
| 20:00 | 4972 | IFK Haninge vs Taby FK | 1.82 | 3.73 | 3.53 |
| 20:30 | 1849 | Hermanstadt vs Botosani | 2.71 | 3.06 | 2.61 |
| 20:30 | 3450 | Storfors Aik vs Skellefteaa FF | 4.62 | 4.03 | 1.57 |
| 21:00 | 1699 | Guillermo Brown vs Santamarina | 1.67 | 3.28 | 5.08 |
| 21:00 | 1963 | Nueva Chicago vs Flandria | 2.32 | 2.81 | 3.20 |
| 21:00 | 2752 | HFX Wanderers FC vs York United FC | 2.20 | 3.05 | 3.15 |
| 21:00 | 3035 | MTK Budapest vs Szeged | 1.40 | 4.60 | 6.80 |
| 21:00 | 3836 | Tristan Suarez vs San Telmo | 1.86 | 3.18 | 4.02 |
| 21:00 | 4080 | Club Almagro vs Temperley | 1.91 | 3.04 | 4.02 |
| 21:00 | 4464 | Sport Boys Association vs Cesar Vallejo | 2.99 | 3.19 | 2.21 |
| 21:00 | 4712 | Liverpool (URU) vs Defensor Sporting | 2.05 | 3.24 | 3.29 |
| 21:30 | 3815 | Atyra FC vs Sportivo Iteno | 1.97 | 3.20 | 3.80 |
| 21:30 | 5614 | Leandro N Alem vs Argentino Merlo | 3.11 | 2.71 | 2.44 |
| 21:45 | 2157 | Sochaux vs Paris FC | 2.05 | 3.21 | 3.56 |
| 21:46 | 2916 | Magdeburg vs Eintracht Frankfurt | 4.49 | 4.03 | 1.70 |
| 22:00 | 4499 | Watford vs Sheffield Utd | 2.31 | 3.14 | 3.04 |
| 22:00 | 4627 | Mitre SdE vs Deportivo Riestra | 2.03 | 3.00 | 3.64 |
| 22:00 | 4793 | Zamalek vs Pyramids | 2.61 | 2.86 | 2.91 |
| 22:15 | 5882 | Breidablik vs IA Akranes | 1.22 | 6.08 | 8.83 |
| 23:00 | 3041 | Fortaleza (COL) vs Bogota FC | 1.68 | 3.57 | 4.48 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo
Jumatatu Agosti 1, 2022
Nipashe



Guardiola: Haaland atafunga UKURASA 21

# Simba SC haizuiliki, haishikiki- Barbara

## ●●● Yatangaza usajili bado unaendelea, leo kuweka hadharani wadhamini wao...

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Simba imekuja na kauli mpya ya msimu wa 2022/23 ambayo itaitwa 'hatuzuiliki hatushikiki', huku ikitangaza kuwa haijamaliza usajili wake na itakwenda kuwatambulisha wachezaji wengine wiki ijayo.

**Akizungumza jana kwenye uzinduzi wa Wiki ya Simba, kuelekea kwenye kilele cha tamasha la Simba Day lililofanyika viwanja wa Zakhem, Mbagala, Dar es Salaam, Ofisa Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo, Barbara Gonzalez (pichani), amesema kuwa safari yake ya kwenda nchini Misri na Morocco ilikuwa ni muhimu mno kwa ajili ya kujipanga kwa msimu unaofuata ambao anaamini utakuwa mzuri kuliko miaka yote, akitamba safari hii timu walioitengeneza ni moto wa kuotea mbali.**

Nimetoka Misri na Morocco na kitu muhimu ilikuwa ni kujipanga kwa msimu unaofuata. Tunarudi kwa nguvu, tunarudi kutetea ubingwa wetu kauli mbiu yetu ni 'We Are Unstoppable', 'Hatuzuiliki Hatushikiki.'

"Tunakuja kupambana, tunakuja kibabe zaidi, tunakuja kuurudisha ubingwa wa Ligi Kuu, azma yetu ya kufika nusu fainali ya michuano ya kimafaifa ipo pale pale msimu unaofuata, tunakuja kurudisha tena Kombe la FA. Msimu huu hakuna kuteleza tena, bado usajili hatujamaliza," alisema.

"Kikosi chetu ni cha kidijitali kitaendelea kutambulisha wachezaji wengine wapya wiki ijayo. Simba msimu unaoanza hatutelezi tena, hatuzuiliki," alisema huku akishangiliwa na mashabiki wengi waliojitokeza kwenye viwanja hivyo, ambapo kabla ya uzinduzi huo kulikuwa na maandamano ya amani yaliyofanywa na wanachama na mashabiki wa Simba.

Naye Mwenyekiti wa klabu hiyo, Murtaza Mangungu, amesema kuwa kwa sababu wanachama, mashabiki wa Simba hupoteza fedha na muda wao kuitetea, kuishangilia na kuhakikisha timu yao inapata ushindi, basi wao kama viongozi wana wajibu wa kusajili kikosi imara cha wapambanaji ili wawe na furaha.

"Hatujamaliza usajili, tumetoka Afrika, sasa tunaangalia usajili kwenye mabara mengine, tutaweka wazi hiyo wiki ijayo," alisema.

Kuhusu uzinduzi wa jezi, Mangungu aliwataka wanachama na mashabiki wa Simba kutokuwa na wasiwasi kwani siku chache watawatangazia ni lini kwa sababu safari hii hazitotoka tena bara la Asia, bali Ulaya, hivyo zitakuwa na ubora mzuri zaidi na kabla ya kilele cha Simba Day zitakuwa zimeshapatikana.



Mwenyekiti huyo pia ametangaza kuwa leo, klabu hiyo itakuwa na shughuli maalum ya kutangaza wadhamini wapya, akisema si mmoja kama wengi wanavyodhani.



Waziri wa Katiba na Sheria, Damas Ndumbaro, akimvalisha mkanda wa ubingwa wa WBF, bondia Seleman Kidunda baada ya kumchapa kwa pointi mpinzani wake, Tshimanga Katompa raia wa DR Congo, katika pambano lililofanyika Uwanja wa Majimaji, Songea, Ruvuma, Jumamosi. **PICHA: SAADA AKIDA**

# Mshtuko Senzo kuacha kazi

**Na Adam Fungamwango**

KAMATI ya Utendaji wa Klabu ya Yanga imeridhia maombi ya Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu, Senzo Mazingiza, ya kutoongeza mkataba mwingine ambao ulimalizika jana Julai 31, hivyo kumteua Wakili Simon Patrick kukaimu nafasi hiyo kwenye kipindi cha mpito.

Taarifa iliyotolewa juzi jioni na klabu hiyo, ilisema kuwa kamati hiyo ambayo ilifanya kikao chake cha kwanza Julai 30, pamoja na mambo mengine yaliyojadiliwa ni pendekezo la Senzo la kutoongeza mkataba tena kwenye klabu hiyo kwa sababu za kifamilia.

Kwenye taarifa hiyo imesema Senzo aliwasilisha maombi hayo akisema kuwa amekuwa mbali na familia yake kwa kipindi cha takriban miaka mitatu, hivyo ameomba kutoongeza tena mkataba mwingine baada ya huo kumalizika.

"Klabu ya Yanga inamshukuru kwa utumishi wake ulio bora hasa mchango wake kwenye eneo la utawala na kumtakia kila la kheri," ilisema taarifa hiyo iliyotolewa na Idara ya Habari na Mawasiliano ya Klabu ya Yanga.

Hata hivyo, kumekuwa na maoni na mawazo mbalimbali kutoka kwa wanachama na mashabiki wa Yanga kuhusu kuondoka kwa Senzo, wengi wakionekana kushtushwa na kuona imekuwa ghafla sana, wengine wakidhani huenda kuna sababu zingine zaidi hiyo.

Suala la kujiuzulu kwake limechukua nafasi kubwa kwenye mijadala mbalimbali, mitandao ya kijamii na kwenye vijiwe vya soka kila mmoja akizungumza lake, lakini wengi wakionekana kusikitishwa na kuondoka kwake.

Senzo raia wa Afrika Kusini alikuja nchini na kujiunga na Simba kama Ofisa Mtendaji Mkuu mwaka 2019 hadi 2020 alipowashangaza na kuwashtua wengi, akiamua kuacha kazi na kutimkia Yanga ambako moja ya kazi kubwa aliyofanya kuweka mazingira ya kuifanya klabu hiyo kuondoka kwenye mfumo wa zamani na kuingia kwenye mfumo wa mabadiliko ya kisasa ya uwekezaji na baadaye kupewa cheo cha Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >